**Majaliwa** awajibu watu wanaobeza maendeleo ya vitu

UKURASA 3



**Kundi** la vibaka lavamia mtaa na kupora fedha, simu

UKURASA 4




Man Utd yaifuata Chelsea kwa Rice

UKURASA 20

Jumamosi Desemba 19, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580434

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Waziri aishukia mifuko ucheleweshaji wa mafao

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MWAMBE AANIKA 'MCHAWI' BIASHARA**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, amesema moja ya vikwazo vinavyosababisha Watanzania kushindwa kupiga...

UKURASA WA 4

**MKEMIA ACHUKUA HATUA KUMALIZA UTATA WA DNA**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), imeanza kuchukua hatua za makusudi kupunguza utata wa kisheria wakati...

## Matatani madai ya kukutwa bunduki nne, risasi 36

UKURASA 3



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi (kulia), akimkabidhi Anna Mkapa cheti, ikiwa ni Shahada ya Heshima ya Udaktari aliyotunukiwa Hayati Benjamin Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu na Mkuu wa kwanza wa chuo hicho, kwenye mahafali ya 11 yaliyofanyika Ukumbi wa Chimwaga, Jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



## Hatimaye viboko vya DC vyalipa

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

MICHEZO SIMBA: PLATINUM HAWANA FIGISU UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Mwambe aanika 'mchawi' biashara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, amesema kuwa moja ya vikwazo vinavyosababisha Watanzania kushindwa kupiga hatua kwenye biashara ni ukosefu wa elimu ya ujasiriamali.

Mwambe aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufungua mkutano wa wadau kuhusu rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo.

Alisema pamoja na matatizo ya ukosefu wa masoko ya bidhaa mbalimbali na mitaji, elimu bado ni kikwazo kikukwa kwa Watanzania katika kuanzisha biashara zao.

"Watanzania bado hii elimu ya ujasilimali ni suala geni kidogo kwetu, leo hii Mtanzania anakwenda chuo cha biashara kusoma ili aje kuwa msimamizi wa biashara ya mtu na si kubuni yake, "alieleza Mwambe.

Kutokana na hali hiyo, alivitaka vyuo vya elimu ya biashara nchini pamoja na taasisi mbalimbali kuweka utaratibu wa kutoa mafunzo ya ngazi mbalimbali ili kuwajengea uwezo watu kwenda kuanzisha biashara zao.

"Leo hii unakuta Chuo cha Elimu ya Biasahra (CBE) kinafundisha mtu kwenda kuwa msimamizi wa biashara ya kampuni fulani lakini yeye mwenyewe si mfanyabiashara. Inabidi tubadilike. Hivi karibuni nilikutana na Mo Dewji akanambia anasoma shahada ya uzamili ya biashara Dubai. Hata sisi wajasiriamali wadogo lazima tusome ili kuwa wafanyabiashara na si wasimamizi," alisisitiza.

Kuhusu rasimu hiyo ya sera ya maendeleo ya viwanda vidogo na biashara ndogo, aliwata wajumbe wa mkutano huo kufanya maboresho ili ipatikane sera itakayosaidia sekta hiyo.

"Lazima mtoke na maboresho ya sera ambayo itakwenda kutambua viwanda vidogo pamoja na biashara ndogo kwani ndizo ambazo zimewatoa watu wengi mtu kama Bakharesa alianza na kutembeza mikate lakini hivi sasa ni tajiri mkubwa" alisema.

Pia alisema serikali imekuja na rasimu ya sera hiyo kutokana na iliyokuwapo awali kuwa ya muda mrefu na haikidhi mahitaji ya sasa.

Alisema sera ya ujasiriamali ni ya mwaka 2003 ni siku nyingi sana inatakiwa kufanyiwa marekebisho ili kwenda kisasa. "Lakini changamoto nyingine katika sera ile ya awali ni ilijengwa katika malengo ya sekta moja tu ya viwanda ndiyo maana akawa zaidi chini ya SIDO, lakini hivi sasa biashara ndogo zipo katika sekta zingine pia kama vile hoteli," alisema.

Mwambe alisema sera hiyo mpya itakuwa na uwezo wa kuwawezesha wajasiriamali wadogo kukua kutoka ngazi ya chini na kuwa wafanyabiasahra wakubwa hali itakayosaidia kuongeza walipa kodi na taifa kupata mapato.



Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenani Kihongosi (kushoto), akimkabidhi Sh. milioni 5.4 Mkuu wa shule ya Sekondari Sinoni, Nteles Lorna, kama fidia ya viti vilivyopotea katika shule hiyo baada ya wanafunzi wa shuleni hapo kuviiba viti hivyo na kuwauzia wafanyabiashara wa vyuma chakavu. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Waziri ashukia mifuko ucheleweshaji mafao

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imeitaka mifuko ya hifadhi ya jamii nchini kuacha ujanja ujanja badala yake ijikite kulipa mafao kwa wakati kwa wanachama wao wanaostaafu ama kuachishwa kazi.

Imeitaka mifuko hiyo kutowazungusha na kuwapa usumbufu usiokuwa wa lazima wanachama wanaofuatilia mafao yao.

Vilevile, serikali imewataka wakurugenzi wa mashirika hayo kuchukua hatua na 'kuwatumbua' wafanyakazi wao hususani mameneja wa mikoa kwa kuwa wanafanya kazi kwa mazoea na wamekuwa wazembe kazini.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenister Mhagama, alitoa maagizo hayo jijini hapa alipofunga semina ya viongozi wa Shirikisho la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (TSSA).

Mhagama alieleza kushangazwa na kitendo cha wafanyakazi wa mifuko ya hifadhi kuwadai barua za miaka 40 nyuma wanachama wao wanaostaafu kama moja ya vielelezo.

"Mtu ana miaka 60 na amestaafu, leo anakuja kufuatilia mafao yake, mfanyakazi wa mfuko wa hifadhi unamdai barua ya miaka 40 nyuma, sasa ataipata wapi? Matokeo yake mnaanza kuwasumbua tu watu na kuwazungusha," alionya.

Mhagama alisema moja ya kazi za mifuko hiyo ni kuweka kumbukumbu za mfanyakazi ambaye ni mwanachama wao kabla ya kufikia umri wa kustaafu, ili ukifika wakati alipwe mafao yake bila usumbufu.

Aliongeza kuwa kazi hiyo inatakiwa kufanywa na maofisa utekelezaji ambao na wanalipwa mishahara, akibainisha kuwa malalamiko ya wanachama katika eneo la mafao yamekuwa mengi.

Kuhusu 'utumbuaji' wa wafanyakazi, Mhagama alisema siku hizi hasikii watu wakiwajibishwa kama ilivyokuwa mwanzo licha ya kuwapo watumishi wazembe wasioendana na kasi ya serikali ya awamu ya tano.

Akizungumzia suala la uwekezaji kwa mifuko hiyo, waziri huyo aliwataka watendaji wa mifuko hiyo kuwa makini ili wawekeze kwa faida badala ya kuingia mikataba mibovu kama ilivyotokea siku za nyuma. Aliwataka watendaji na wenyeviti wa bodi za mifuko hiyo kuwa makini na suala hilo ili kusaidia nchi kujenga uchumi na kuinua maisha ya Watanzania. Mhagama pia aliitaka mifuko hiyo kufanya tathmini ya kina ili kuongeza wanachama kwa kuwa kwa sasa ni asilimia 4.3 pekee ya watumishi ndiyo wanachama wao.

Aliongeza kuwa asilimia 56 ya vijana wote hawako katika mifuko na kwamba kuna haja ya kuongeza nguvu katika upande huo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa TSSA, William Erio, akizungumza katika semina hiyo, alisema mifuko hiyo ipo tayari kushirikiana na serikali katika kuwekeza hususani kwenye viwanda.

Alisema mifuko yote imeanza kuchukua hatua na kwamba suala hilo litaleta tija kwa nchi na wanachama wao ambao wanachangia michango yao.

# Walionunua madawati 500/- walipa mil. 5.4/-

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

SIKU moja baada ya Mkuu wa Wilaya ya Arusha kuwacharaza viboko wafanyabiashara wa vyuma chakavu waliodaiwa kununua madawati yaliyoibwa shuleni, wamiliki wa biashara hizo wametoa Sh. milioni 5.4 kufidia ya viti vilivyoibwa.

Desemba 16, mwaka huu, Mkuu wa Arusha aliwacharaza viboko hadharani wafanyabiashara wa vyuma chakavu pamoja na wanafunzi watatu kwa kosa la kuuza viti vya shule kama vyuma chakavu.

Akipokea fedha hizo jana, Mkuu huyo wa wilaya, Kenan Kihongosi, alitoa siku saba kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Sinoni kuhakikisha viti na meza vinapatikana kwa ajili ya wanafunzi wa shule hiyo.

"Mkuu wa shule hizi fedha ndani ya siku saba viti vya wanafunzi viwe vimekamilika na tunajua kiti kimoja ni 50,000 na meza 50,000 jumla ni Sh. 100,000 hivyo jumla ya viti na meza 108 gharama ni 5,400,000," alisema.

Alitoa rai kwa maofisa elimu wilayani hapo kufanya uhakiki wa samani za shule ili kujiridhisha kama kuna madawati ya kutosha wanafunzi kama yalivyotolewa na serikali.

Pia, aliwataka wananchi, wafanyabiashara kuwa wazalendo wa nchi yao na kutoa taarifa sehemu husika ili kuendelea kulinda rasilimali za nchi.

Alisema kuwa baada ya watuhumiwa waliohusika na ununuzi wa vyuma chakavu kukamatwa, waliomba kusamehewa na kuahidi kutoa fedha za kulipa viti hivyo ambapo jana walikabidhi kiasi hicho cha fedha.

Mmiliki wa biashara ya vyuma chakavu, Yuda Kamando, alikiri kuwapo na makosa katika ofisi yake ambapo aliomba kusamehewa na kuahidi kutoa ushirikiano kwa serikali kwa kila hatua.

"Nikiri wazi kuwa kweli ofisi yangu yalijitokeza makosa ya kununua vyuma vitokanavyo na viti vya shule. Mimi sikuwapo lakini vijana wangu walinunua mzigo bila kujua kama bado vilikuwa katika matumizi, " alisema Kamando.

Alisema watatoa elimu kwa vijana wanaonunua vyuma ili kuhakikisha wananunua vile vinavyostahili kununua na siyo vinginevyo kwa kuwa kufanya hivyo ni kujiharibia jina katika biashara na kuendelea kujiingiza katika matatizo.

Diwani wa Sinoni, Michael Kivuyo, alisema ni jambo jema wamiliki hao kulipa fedha kwa ajili ya watoto kupata madawati ya kukaa wawapo shuleni kwa kuwa Januari watoto wanapaswa kuendelea kusoma.

Aliwataka wamiliki wa biashara za vyuma chakavu kuacha kununua au kuwatuma watoto kuokota chuma na wakibainika kuendelea kufanya biashara hiyo na watoto, hatua za kisheria zitachukuliwa.

# Majaliwa awajibu wanaobeza maendeleo ya vitu



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akitazama mahali panapochimbwa ili kusimika moja ya nguzo za daraja la Kigongo, Busisi wakati alipokagua ujenzi wa daraja hilo mkoani Mwanza jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa , amezijibu kejeli za wapinzani wao wa kisiasa kwamba serikali imekuwa ikifanya maendeleo ya vitu badala ya watu, akisisitiza kwamba miradi mikubwa ya kimkakati itasaidia kukuza uchumi.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana alipotembelea na kukagua ujenzi wa daraja la JPM linalounganisha Wilaya za Sengerema na Misungwi mkoani Mwanza.

Waziri Mkuu alikagua ujenzi wa daraja hilo lenye urefu wa Km 3.2 na barabara unganishi, sasa ukiwa umefikia asilimia 12. "Tanzania ni nchi yenye changamoto ya ajira, Serikali inaendelea kujenga miradi mikubwa ya kimkakati kwa ajili ya kupunguza ugumu wa suala hili, kwa kuwatumia wananchi wa maeneo husika katika miradi, ujenzi wa daraja hili ambalo ni la kwanza kiukubwa, umeajiri wazawa zaidi ya 370," alisema.

Majaliwa alisema daraja hilo la Kigongo-Busisi linajengwa na Kampuni ya China Civil Engineering Group Limited kwa gharama ya Sh. bilioni 699.2.

Aliongeza kuwa ujenzi wa daraja hilo ni mwendelezo wa ujenzi wa madaraja mengine nchini na kwamba serikali inatumia fedha za ndani.

Majaliwa pia alikagua miradi ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Buhongwa na ujenzi wa MV Mwanza Hapa Kazi Tu. Akiwa katika shule hiyo, Waziri Mkuu alishuhudia upungufu wa vyumba vya madarasa huku Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Kiomoni Kibamba, akiahidi ifikapo Januari 11, mwakani, vyumba vyote vitakuwa vimekamilika.

"Ninakuahidi mkuu, ifikapo Januari 11, mwaka ujao, vyumba vyote vitakuwa vimekamilika na wanafunzi wataendelea na masomo yao," alisema.

# Mbaroni madai kukutwa silaha nne, risasi 36

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

JESHI la Polisi Mkoani Shinyanga, linamshikilia Masanja Bugolole (75), mkazi wa kijiji cha Gula wilayani Kahama, kwa tuhuma za kumiliki silaha nne aina ya Shotgun na risasi 36 kinyume cha sheria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magiligimba, akizungumza jana na waandishi wa habari mjini hapa, alisema Bugolole amenaswa kutokana na misako maalum inayoendelea dhidi ya wahalifu wa makosa mbalimbali.

Magiligimba alisema juzi, majira ya saa 6:30 usiku, askari walimkamata mtuhumiwa huyo nyumbani kwake akiwa na silaha hizo.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa na silaha nne, mojawapo ikiwa na usajili wa namba TZCAR 34951 ambayo namba zake zimefutika.

Kamanda alisema silaha tatu zisizo na usajili ni zenye namba D172321, namba 14999 na namba 24162.

Licha ya silaha hizo, Kamanda Magiligimba alisema kuwa mtuhumiwa huyo alikuwa na mitutu sita ya silaha aina ya shotgun pamoja na kifaa kingine cha jadi kinachotumia moto kukoleza silaha hizo.

Kamanda Magiligimba aliwaeleza waandishi wa Habari kuwa Mtuhumiwa huyo atafikishwa Mahakamani mara baada ya upelelezi kukamilika ili ajibu tuhuma zinazomkabili.

Katika hatua nyingine, Kamanda Magiligimba alisema Desemba, 9 mwaka huu, majira ya saa 1:00 jioni, askari wakiwa doria katika kijiji cha Mpela wilayani Kahama, waliokota bunduki aina ya gobore ikiwa imetelekezwa kwenye kichaka.

Kutokana na hali hiyo, Kamanda Magiligimba aliwataka wananchi mkoani Shinyanga kuendelea kutoa taarifa za siri zitakazofanikisha kukamatwa kwa wahalifu wengine wa makosa ya namna hiyo.

Sambamba na hilo, kamanda huyo aliwataka watu wote wenye nia ovu kutafuta mali kwa njia halali.

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
AT KISUTU

CIVIL CASE NO. 17 OF 2020

MM INDUSTRIES LTD..........................PLAINTIFF
VERSUS
HBM IMPORT & EXPORT LTD-----...........----DEFENDANT

NOTICE OF DATE OF JUDGMENT

**TAKE NOTICE** that, the above mentioned case has been fixed for Judgment on the 22th day of December 2020 At 01:00 pm.

**YOU** are required to appear in this Court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to relay in support of this case.

**GIVEN** under my hand and the **SEAL** of the Court this 16th day of December 2020.

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
KISUTU – DAR ES SALAAM

TO BE SERVED UPON

The Managing Director,
HBM IMPORT & EXPORT LTD
TANZANIA

# Mkemia achukua hatua kumaliza utata wa DNA

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), imeanza kuchukua hatua za makusudi kupunguza utata wa kisheria wakati wa uchukuaji wa sampuli za vinasaba (DNA) katika masuala yanayohusisha matibabu na makosa ya jinai.

Jana, Mkurugenzi wa Huduma za Sayansi Jinai wa GCLA, David Elias, alisema nia ni kuhakikisha wadau mbalimbali wakiwamo madaktari na polisi wanapochukua sampuli hizo na kuzipeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali wanatekeleza jukumu hilo kwa usahihi, uhifadhi mzuri na kusafirishwa kwa muda unaotakiwa.

Elias alikuwa akitoa mada kwa wanafunzi wa mwaka wa tano wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba cha Kilimanjaro Christian Medical College (KCMCo) na madaktari wa Hospitali ya Rufani ya Kanda (KCMC).

Alisema hivi sasa serikali imejipanga kuwa na vyombo, mitambo ya kisasa na wataalamu wa kutosha waliobobea katika utoaji wa majibu kwa wakati na ya uhakika.

"Kwa kutambua umuhimu wa Ofisi ya Mkemia Mkuu, serikali imeamua kufungua ofisi katika kanda sita nchini ili kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi.

"Madaktari na polisi hawana budi kutumia ofisi za Mkemia Mkuu wa Serikali za kanda ili kurahisisha utoaji matokeo ya kiuchunguzi kwa haraka," alisema.

Alisema kwa mwaka huu peke yake, GCLA imefanya uchunguzi wa kisayansi kwa kupima sampuli zinazohusiana na masuala ya jinai 7,000.

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pia inasimamia utekelezaji wa Sheria tatu ambazo ni Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali Na. 3 ya Mwaka 2003, Sheria ya Vinasaba vya Binadamu (HDNA) Na. 8 ya Mwaka 2009 na Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Na. 8 ya Mwaka 2016.

Mwanasheria Mkuu wa Mamlaka hiyo, Miriam Mvano, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo kwa wanafunzi wa udaktari kwa kuwa katika uchunguzi wa vinasaba kuna uhusiano kati ya Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na madaktari katika uchunguzi unaohusiana na matibabu na makosa ya jinai.

Alisema mkakati huo utasaidia kuhakikisha sampuli zinazochukuliwa kuleta matokeo sahihi yanayofanana kwa muda na wakati unaotakiwa.

"Hapa tunaelimisha madaktari wakienda kazini katika vituo vyao vya kazi, wakumbuke ushiriki wao na Ofisi ya Mkemia Mkuu wakati wanapotekeleza majukumu yao ya uchunguzi wa afya na matibabu, ama polisi wanapochukua sampuli za dawa za kulevya kwa usahihi," alisema mwanasheria huyo.

Akizungumza baada ya mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo, mwanafunzi wa udaktari, Kaisi Katope, aliishauri serikali kuandaa mitaala maalum ya kufundishia kuhusu taratibu za sheria na kanuni za kisera za uchukuaji sampuli kwa ajili ya uchunguzi.



Mkurugenzi wa Shirika la UDIDA Mkoani Shinyanga, Jasson Kyaruzi (kulia), ambao wanajishughulisha na shughuli za kijamii, akikabidhi mifuko 15 ya Saruji kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Town iliyopo Manispaa ya Shinyanga, Jasson Rwegasira, kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya vyumba vya madarasa jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Kundi la vibaka lavamia mtaa na kupora mali

**Na Romana Mallya**

KUNDI la vijana wenye silaha za jadi limevamia nyumbani za wakazi wa Majohe, Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam na kuwajeruhi baadhi yao huku wakiwapora simu na fedha.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ilala, Kamishna Msaidizi (ACP) Janeth Magomi, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi majira ya saa 8:00 usiku.

"Ni kweli tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Alhamisi. Kikundi cha vibaka kiliingia katika baadhi ya nyumba wakawa wanapora simu na fedha kutoka kwa wananchi. Nilifika eneo la tukio na wahanga (waathirika) waliojeruhiwa ni watatu.

"Majeruhi wa kwanza yupo Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI) anaendelea na matibabu na mwingine alipelekwa Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe Mkoa wa Pwani na mwingine tulimkuta nyumbani akiwa na majeraha," alisema.

Magomi alisema baada ya tukio hilo walifanya operesheni na kuwakamata vijana wawili wanaotuhumiwa kuhusika na tukio hilo.

"Kikundi hiki tumeshakibaini na wale tuliowakamata wanatuambia waliofanya nao tukio hili. Idadi yao hawajatueleza lakini tunajua, walikuwa wanatumia silaha za jadi ambazo ni mapanga," alisema.

Kamanda huyo alisema kikundi hicho baada ya kufika eneo hilo, kilikwenda kwenye nyumba ya mwanajeshi ambaye alipotoka walimwambia wanamheshimu na wanamjua.

"Ndiyo maana tuliweza kubaini hawa ni vijana wa hapo hapo mtaani. Hakuna mwanamke aliyejeruhiwa katika tukio hili," alisema.

# RAS kuchunguza biashara kusafirisha watoto

**Na Francis Godwin,** IRINGA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Iringa, Hapiness Seneda, amesema uongozi wa mkoa unafuatilia taarifa za uwapo wa biashara haramu ya kusafirisha watoto kwenda kufanya kazi nje ya mkoa pamoja na mtandao wake.

Amesema iwapo itabainika kuwapo watu na mtandao unaojihusisha na vitendo hivyo, hatua kali zitachukuliwa.

Akizungumza jana wakati wa kikao cha kamati ya uchaguzi wa wanafunzi waliochaguliwa kijiunga na kidato cha kwanza mapema mwakani, Seneda alisema mkoa ulikwisha piga marufuku wazazi kuruhusu watoto waliomaliza elimu ya msingi au sekondari kwenda mijini kutumikishwa kwenye kazi za ndani.

Seneda alisema ofisi yake imepokea taarifa za mwananchi anayedaiwa kusafirisha mtoto mmoja kwenda nje ya mkoa kufanya kazi za ndani, jambo ambalo alisema ni kinyume na mikakati ya ulinzi wa mtoto iliyowekwa na serikali ya mkoa wa Iringa.

Pasipo kutaja jina la mtuhumiwa wa biashara hiyo, Katibu Tawala huyo alisema viongozi wote wa mkoa kuanzia ngazi ya kijiji wana wajibu wa kuweka ulinzi wa kutosha kwa watoto waliomaliza elimu ya msingi na sekondari kuhakikisha wanabaki vijijini kuendelea na elimu ya sekondari au ufundi na si kuwaruhusu kwenda mijini kutumika katika kazi za ndani .

Kuhusu matokeo mazuri ya mtihani wa darasa la saba uliofanyika mwaka huu, Seneda alisema yametokana na jitihada mbalimbali ambazo zimefanywa na wadau wa mkoa wakiwamo walimu, wazazi na viongozi wote wa ngazi za jamii.

"Kwa kuzingatia matokeo mazuri ya ufaulu wa mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2020 katika mkoa wetu, naelekeza wakurugenzi kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaripoti shuleni na kuanza masomo mara shule zitakapofunguliwa Januari 11, mwakani.

Kwa awamu ya kwanza, wanafunzi 907 wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa wahakikishe wanaripoti kabla ya Februari 28, 2021," alisema.

"Wakurugenzi pia wahakikishe mikutano ya tathimini ya elimu inafanyika katika halmashauri zote na kutafuta sababu za kufanya vibaya kwa baadhi ya shule katika mitihani hatimaye kutafuta ufumbuzi kwa kuweka mikakati endelevu," alisisitiza.

Seneda pia aliagiza kila halmashauri ihakikishe inafanya mapitio ya mwenendo wa ongezeko la ufaulu wa wanafunzi waliojiunga na kidato cha kwanza uendane na madarasa pamoja na madawati (viti na meza).

Alisema kila halmashauri ihakikishe inafanya usimamizi na ufuatiliaji wa ufundishaji na ujifunzaji kuona unakuwa wa karibu zaidi na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara shuleni ili kuondoa ufaulu wa daraja la sifuri na daraja la nne .

Katika hatua nyingine, katibu tawala huyo aliwatangaza wanafunzi wote 23,297 wakiwamo wavulana 11,180 na wasichana 12,117 kuwa wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa awamu mbili kuanzia Januari, mwakani.



Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti Tanzania (TARI), Dk. Geoffrey Mkamilo, kuhusu mifuko maalum ya kuoteshea miche bora ya michikichi juzi katika ziara yake katika kituo mahiri cha utafiti wa zao hilo (TARI Kihinga) mkoani Kigoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanne kizimbani tuhuma za wizi

**Na Halfani Chusi**

MENEJA wa Azam Huduma kwa Wateja, Roth Mziray, na wenzake watatu, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na mashtaka ya wizi na kuhamasisha wizi.

Katika kesi hiyo iliyofunguliwa mahakamani huko chini ya Hakimu Lyamuya, Meneja wa Azam, Mziray anakabiliwa na shtaka la kushindwa kuzuia wizi akidaiwa kutumia madaraka yake vibaya na kusababisha kumilikisha mtu mwingine mali ya wizi kinyume cha sheria.

Washtakiwa wengine katika shauri hilo namba 439/2020 ni: Nicholous George, anayeshtakiwa kwa makosa mawili ya kuvunja na kuiba mali; Frank Mnyagizi Ishengoma, anayekabiliwa na mashtaka mawili ya wizi na kusaidia kufanikisha wizi; Frank alikuwa mfanyakazi wa Wakala wa Azam Media uitwao Elgod Professional Ltd.

Wakili wa Serikali, Deborah, akisoma hati ya mashtaka, alidai kuwa mnamo Agosti 18, 2016, katika maeneo ya Mbezi Msigani, Wilaya ya Ubungo jijini, washtakiwa hao kwa nafasi zao tofauti walishirikiana kuvunja na kufanikisha kuiba mali zenye thamani ya Sh. milioni 3.2 kiambaza aina ya Sony, DVD aina ya Sony, pasi aina ya Philips na vifaa vya muziki, mali ya Godo Biwi.

Hata hivyo, washtakiwa hao walikana mashtaka hayo na hakimu kuahirisha kesi hiyo hadi Desemba 28, mwaka huu itakapoanza kusikilizwa.

Baada ya kuahirishwa kwa shauri hilo, washitakiwa watatu wamerudishwa rumande kutokana na kushindwa kukamilisha utaratibu wa dhamana.

# Utafiti: Maji hayajapungua ardhini

**Na Frank Monyo**

MJIOLOJIA Mkuu kutoka Mamlaka ya Maji Dodoma (DUWASA) Idara ya Rasilimali za Maji, Emmanuel Nahozya, amesema utafiti unaonyesha hakuna dalili za kupungua kwa maji chini ya ardhi katika jiji hilo.

Hiyo inatokana na mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo yaliyofanyiwa utafiti kuwa na vyanzo vya maji, kutunzwa na kuhifadhiwa vizuri na kufanya maji ya mvua kuhifadhiwa kwenye miamba.

Nahozya aliyasema hayo alipowasilisha Tathimini ya Utunzaji wa Rasilimali za Maji katika jiji hilo, ikiwa ni mkakati wa kulinda na kutunza vyanzo vya maji kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa Dodoma.

Alisema kulingana na wingi wa ongezeko la watu katika jiji hilo, vimetafutwa vyanzo vingine vya maji ambavyo zitasaidiana na vilivyopo ili kuongeza uzalishaji wa maji katika jiji hilo ili kuendana na kasi ya matumizi ya maji.

"Kuna visima vimechimbwa vya uchunguzi kwa ajili ya kuangalia uwiano wa maji katika Bonde la Makutupola kwamba yanashuka au yanapanda kwa kadri tunavyotoa maji mengi, hivyo inatoa mwanga ni kiasi gani cha maji tulichonacho," alisema.

Aliongeza kuwa kazi ya Idara ya Rasilimali za Maji kupitia kwenye mabonde ni kutunza vyanzo vya maji ili viendelee kuwa endelevu kwa vizazi vya sasa na vya baadaye.

"Kutunza rasilimali za maji ni pamoja na kuzuia ufyekaji na ukataji miti ovyo, matumizi mabaya ya ardhi kwa kufanya shughuli za kilimo kwa kutumia mbolea zenye kemikali na vitendo vyote vya kibinadamu katika eneo la bonde hilo ambavyo vitasababisha maji chini ya ardhi kupungua," alisema.

**"Kutunza rasilimali za maji ni pamoja na kuzuia ufyekaji na ukataji miti ovyo, matumizi mabaya ya ardhi kwa kufanya shughuli za kilimo kwa kutumia mbolea zenye kemikali na vitendo vyote vya kibinadamu katika eneo la bonde hilo ambavyo vitasababisha maji chini ya ardhi kupungua," alisema.**

Mtaalamu huyo alisema Wizara ya Maji kupitia Idara ya Rasilimali za Maji Dodoma na kwenye mabonde imekuwa ikisimamia kwa karibu utunzaji na usimamizi wa bonde hilo ili kukabiliana na hali hiyo.

Aliongeza kuwa kazi iliyofanyika katika Idara ya Rasilimali za Maji Dodoma ni kufanya tathmini ya uwezo na wingi wa maji yaliyopo katika Bonde la Makutupola na kufanya utafiti kuna maji kiasi gani na yanaweza kutumika kwa muda gani.

"Kwa sasa hivi tumejaribu kusimamia utoaji wa maji yanayovia ardhini kila mwaka yawe sawa sawa na yanayotolewa kwani ukitoa maji mengi tofauti na yanayokuwa 'recharged', maji yatapungua," alisema Nahozya.


**TWINS AUCTION MART CO LTD & COURT BROKER**
P.O.Box1305 Songea,
Head Office: Nssf Building Room No.12 & 13 Songea,
Branch Office 2th Floor Mbinga Stand Room No 105 Mbinga, Makambako Near Sabbath Church Mlando Street,Capri Point Mwanza Town and Arusha branch Imalaseko kilombero.
Mobile: 0716070298/0754881926/0784718734.Email:twinscoltd@gmail.Com
website www.twinsauctionmart.coltd

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA LEO 19/12/2020**

**KWA IDHINI TULIYOPEWA NA MUCOBA BANK PLC MAFINGA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU WA MUCOBA BANK PLC MAFINGA. MNADA UTAFANYIKA TAREHE 21/1/2021 SIKU YA ALHAMISI NA KUENDELEA KUANZIA SAA 4:10 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI ZILIPO DHAMANA ZA WADAIWA,WADAIWA HAO NI HAO WAFUATAO:**

| NA | JINA LA MDAIWA | DAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
|---|---|---|---|
| 1. | BEN JACKOB MAHENGE | NYUMBA KIWANJA NA.444 KITALU 3Q | KIWANJA NAMBA 444 KITALU 3Q MWEMBE TOGWA - IRINGA |
| 2. | RUTH LUCAS MATOWO | NYUMBA | MTAA WA BLOCK "J" MAFINGA |
| 3. | WAZIRI ATILIO LUHANGA | NYUMBA | IGOMBAVANU |
| 4. | MARY FRANCIS NGELULA | NYUMBA | KIWANJA NAMBA 586 KITALU "D" - MAFINGA |
| 5. | TADEI BENARD SANGA | NYUMBA | KITWIRU - IRINGA |
| 6. | DICKSON CHARLES MASASI | MSINGI WA NYUMBA | KIWANJA NAMBA 123, KITALU"A" MAKALALA. |
| 7. | ELKAGHA ISACK SANGA | NYUMBA | MTAA WA AMANI - KINYANAMBO |
| 8. | ESTER MUSSA LUHANGA | NYUMBA | IHONGOLE - MAFINGA |

**NB: MASHARTI YA MNADA:**

MNUNUZI ATAKAEBAHATIKA ATATAKIWA KULIPA 25% YA BEI ILIYOFIKIWA PAPO HAPO. NA KIASI KILICHOBAKI KILIPWE NDANI YA SIKU 14, KINYUME CHA HAPO PESA ILIYOTOLEWA AWALI HAITA RUDISHWA, NA MNADA UTARUDIWA TENA.
GHARAMA ZA KUBADILISHA HATI MILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE,NA GHARAMA ZA KWENDA KUANGALIA/ KUKAGUA NYUMBA/MASHAMBA,BAJAJI/VIWANJA NI ZA MTEJA MWENYEWE. IKUMBUKWE KWAMBA MDHAMINI NI SEHEMU YA MKOPAJI.
LIPA DENI LAKO KABLA YA TAREHE 21/01/2020 UKISUBIRI MPAKA SIKU YA MNADA GHARAMA ZITAONGEZEKA TSH.100,000/= **WOTE MNAKARIBISHWA**

***Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na:-***
MKURUGENZI
S.L.P. 1305,
SONGEA
**SIMU NA. 0754881926,0716070298.**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu ziwe makini mikataba wachezaji wa mkopo Bara

**KLABU** za Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, zipo katika harakati za kuimarisha vikosi vyao, baada ya dirisha dogo la usajili kufunguliwa tangu Jumatano Desemba 16 huku likitarajiwa kufungwa Januari 15, mwakani.

Tunafahamu katika kipindi hiki cha timu kujiimarisha wapo baadhi ya wachezaji watatemwa ili kutoa nafasi kwa nyota wapya ambao klabu husika zinaamini wanaweza kuzisaidia kutimiza malengo yao, lakini pia wapo ambao waliotolewa kwa mkopo klabu zao zitahitaji kuwarejesha huku wengine wakitolewa pia kwa mkopo.

Katika hilo, tunakumbuka vema mvutano mkali uliotokea usajili wa dirisha dogo lililopita kwa Azam FC ilipotaka kumrejesha mshambuliaji wake, Ditram Nchimbi kutoka Klabu ya Polisi Tanzania ili kumuuza Yanga.

Nchimbi ambaye alikuwa akiichezea Polisi Tanzania kwa mkopo ulioelezwa kuwa wa msimu mzima, lakini klabu yake mama, Azam ilitaka kumrejesha kabla haujamalizika ikitaka kumuuza Yanga, ndipo pakazuka mvutano mkali. Kwa mujibu wa Polisi Tanzania, makubaliano yao na Azam yalikuwa kumtumia mchezaji huyo hadi mwishoni mwa msimu ndipo arejee klabuni kwake, na hapakuwa na kipengele chochote kinachoiruhusu Azam kumchukua katikati ya msimu, jambo ambalo liliifanya kupaza sauti za kumzuia kuuzwa Yanga kabla ya baadaye kuketi na kuyamaliza kiutu uzima.

Lakini kwa upande wa Azam FC ilieleza kwamba hapakuwa na kipengele chochote kinachoeleza kwamba hawataruhusiwa kumchukua mchezaji wao watakapomhitaji, huku wakiamini ni sawa na mtu kumpa mtoto wako akulelee, jambo ambalo unapomhitaji unaweza kumchukua wakati wowote.

Azam ilieleza baada ya Yanga kufika dau la kumnunua Nchimbi, ilitoa kipaumbele kwa Polisi Tanzania kama inamhitaji jumla imnunue, lakini ikawaeleza haina uwezo huo na kuwaruhusu kuendelea na taratibu zingine za kumuuza, lakini baadaye pakazuka mvutano wa kumwachia. Tumelazimika kukumbusha sakata hilo hasa kipindi hiki ambacho klabu zipo sokoni kuimarisha vikosi vyao huku kukiwa na idadi kubwa ya wachezaji kutoka klabu kubwa nchini waliowekwa kwenye orodha ya kutolewa kwa mkopo.

Hatutaki kuona tena mvutano kama huo wa Azam FC na Polisi Tanzania ukijitokeza kwa wachezaji watakaotolewa kwa mkopo pindi klabu mama itakapohitaji kuwarejesha ama kuwauza.

Hivyo, katika hilo mbali na kuzitaka klabu kulizingatia, lakini pia Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), linapaswa kuwa makini kwenye suala zima la mikataba ya wachezaji hususan hawa wa mkopo si tu kwa ajili ya kuepusha mvutano kama huo bali pia kusaidia kulinda maslahi ya pande zote pamoja na mchezaji husika.

Utata uliojitokeza katika mkataba wa mkopo wa Nchimbi ni wazi makubaliano mengi ya klabu zetu inaonekana yanafanywa kwa mdomo zaidi badala ya kuwekwa katika maandishi, hivyo klabu zinapaswa kubadilika na kuendesha mambo yao kisomi zaidi, lakini pia TFF inapaswa kuhakikisha vipengele vyote muhimu vinazingatiwa kabla ya kuipokea mikataba ya wachezaji. Tunatambua mikataba ya mikopo kwa wachezaji huwa ina vipengele vingi muhimu na huwa hawatolewi kiholela kama ambavyo klabu zetu nchini zinafanya, kwani; awali kabisa, ni lazima mkopo huo uainishe wazi ni wa muda gani na nani atamlipa mshahara mchezaji husika.


Kingine cha kuzingatiwa katika mkataba wa mkopo unaweza kuwa na kipengele kwa klabu mama kumhitaji mchezaji wao muda wowote ama hatoruhusiwa kucheza dhidi ya klabu yake hiyo pindi timu hizo zitakapokutana, lakini pia pindi itakapotaka kumuuza, klabu anayoichezea kwa mkopo itapewa nafasi ya kwanza ya kumnunua na ikishindwa ama kutohitaji tena huduma yake ndipo auzwe kwingineko.

Hayo ni machache tu katika mengi yanayopaswa kuwekwa wazi kimaandishi katika mikataba ya wachezaji wanaotolewa kwa mkopo, hivyo wakati huu usajili ukiendelea, TFF haina budi kuhakikisha wanachama wake ambao ni klabu wanafuata taratibu zote zinazopaswa kabla ya kuwaidhinisha wachezaji husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Akupaye kisogo si mwenzako

**ANAYEKUONESHA** au kukugeuzia shingo (kukupuuza) si mwenzako. Ni methali inayotunasihi umuhimu wa kuwatambua tunaoweza kuwategemea na tusioweza kuwategemea.

Je! Simba na Yanga zilizo jiji moja lililoitwa Bandari ya Salama katika nchi iliyojulikana kwa jina la Tanganyika, lakini kwa kutaka umoja wa kidugu na Zanzibar sasa yaitwa Tanzania, zajua thamani ya udugu?

Badala ya kupendana kama ndugu wa nchi moja, zachukiana kama walivyo Waarabu na Waisraeli ingawa wote ni waja, yaani watu wa Mwenyezi Mungu!

"Kuchukiana huondokesha fitina, bali kupendana husitiri makosa yote. Yeye afichaye chuki ana midomo ya uongo, na yeye asingiziaye ni mpumbavu. Katika wingi wa maneno hapakosi kuwa na maovu, bali yeye azuiaye midomo yake hufanya akili." (Mithali 10:12, 18-19).

Simba na Yanga ndizo timu zenye wanachama na mashabiki wengi kuliko timu yoyote ya kandanda nchini. Pia zajulikana zaidi katika Bara la Afrika kwani ndizo timu za Tanzania zilizocheza na zinazocheza zaidi na timu za ughaibuni (nchi zilizoko mbali na nchi ya mtu).

Ndizo timu zinazosajili wachezaji wengi wa kigeni. Zimekuwa zikisajili wachezaji kutoka Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Zambia, Malawi, Zimbabwe, Congo (DR), Msumbiji, Angola na hata Brazil.

"Fedha ilivunja nguu, milima ikalala." Maana yake pesa zina uwezo wa kuivunja milima na vilima. Methali hii hutumiwa kupigia mfano uwezo wa fedha. Mtu akiwa na pesa anaweza kufanikiwa kufanya mambo ambayo asingeweza kufanya wala kudhania kuyafanya.

Simba na Yanga ndizo timu zenye wanachama na mashabiki wengi kuliko timu zote za kandanda nchini. Hata zinapokwenda kucheza na timu za mikoa mingine, hushangiliwa mno na watu wa mikoa hiyo kuliko timu zao za nyumbani!

"Chako ni chako, cha mwenzako si chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine.

"Ndugu mui afadhali kuwa naye." Maana yake ni afadhali kuwa na ndugu yako hata kama ni m-baya. Methali hii hutumiwa kutunasihi tuwathamini ndugu zetu hata kama wana sifa mbaya kiasi gani. Ndugu yako aweza kukufanyia hisani ambayo rafiki hawezi.

Simba na Yanga ndizo timu zinazovuta watazamaji wengi mikoani na kuzifanya timu za mikoa hiyo kupata hela nyingi kuliko zichezapo na timu zingine!

"Pendo lisiwe na unafiki; lichukieni lililo ovu, mkiambatana na lililo jema. Kwa pendo la ndugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu;" (Warumi 12:9).

Turudi kwa Simba na Yanga ambao mimi nachelea kuziita 'watani wa jadi' kwani chuki (hali ya kutokuwapo upendo, hali ya kuwa na roho mbaya, hali ya kuwa na kinyongo) kati yao yanifanya niziite 'wapinzani wa jadi' si vinginevyo.

Nalazimika kuziita Simba na Yanga 'wapinzani wa jadi' kutokana na vitendo wanavyofanyiana kama Waarabu na Waisraeli (Wayahudi). Ingawa zote ni za Tanzania na kuwa zamani zilikuwa moja kabla ya kutengana kwa takribani miaka 85 iliyopita, vitendo wanavyofanyiana ni chuki, yaani hisia ya kutopenda kitu au jambo.

"Waarabu wa Pemba hujuana kwa vilemba." Maana yake Waarabu wa Pemba hutambuana kutokana na vilemba wanavyovaa.

Methali hii yatukumbusha kuwa watu wanaohusiana au wenye sifa sawa hupatana au huingiliana vizuri mtu wa kando hawezi kuwaingilia. Ni kweli lakini si kwa Simba na Yanga! Kama ndivyo, kwa nini wasiitwe 'wapinzani wa jadi?'

Kama ni kuchekana zinaposhindwa na timu za nyumbani (Tanzania), hakuna shida lakini kuchekana wakati mojawapo imeshindwa na timu ngeni kutoka nje ya nchi ni kudhihirisha umbumbumbu (ufahamu mdogo wa mambo) wao!

"Wapenzi, msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu;" maana imeandikwa: "Kisasi ni juu yangu mimi; nitalipa." Anena Bwana.

"Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema."(Warumi 12:19, 20).

'Wivu' ni neno lenye maana mbili. Kwa muktadha ninaoujadili, ni hali ya kuwa na kinyongo au kijicho wakati mtu aonapo mali, mafanikio au maendeleo ya mtu mwingine; ngoa.

Kati ya Simba na Yanga ni ipi iliyojiendeleza au inayojiendeleza yenyewe kwa fedha za wanachama wake? Jibu ni HAKUNA! Zote zategemea mbeleko/ubeleko/uweleko yaani nguo inayotumika kubebea mtoto mgongoni kwa kupigwa fundo kifuani.

# Atelekeza agizo la JPM kuvutia wawekezaji

**Na Romana Mallya**

BALOZI wa Tanzania nchini Uturuki, Prof. Elizabeth Kiondo, amewapeleka wawekezaji watano kati ya 10 katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ambao wameonyesha nia ya kuwekeza katika viwanda vya kuzalisha zana za kilimo, vifaa tiba na dawa.

Rais John Magufuli mara kwa mara amekuwa akiwataka mabalozi wanaowakilisha Tanzania nchi mbalimbali duniani pamoja na mambo mengine wahakikishe wanahamasisha wageni kuja kuwekeza katika viwanda.

Akizungumza jana na waandishi wa habari baada ya kikao chao kilichohusisha TIC na wadau wa uwekezaji Tanzania, Balozi Kiondo alisema wawekezaji wengi wameonyesha nia ya kuwekeza Tanzania na wako waliofanya hivyo.

"Leo (juzi) nimekuja na wawekezaji watano kati ya 10 ambao nao wametaka kuja kuwekeza katika viwanda vya nguo, zana za kilimo na maeneo matatu ya viwanda vya kuzalisha zana za kilimo, nguo na nepi za watoto," alisema.

Alisema kikao hicho cha siku moja kilihusisha Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Mauzo ya Nje (EPZA), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

Mpaka sasa, alisema waliowekeza Tanzania kutoka nchi hiyo, wengi wamejikita katika sekta ya ujenzi na kilimo.

"Walitarajiwa kuja wawekezaji 10 lakini leo (juzi) wamekuja watano, waliobaki watakuja baadae," alisema.

Mkurugenzi wa Uhamasishaji Uwekezaji TIC, John Mnali, alisema wamepokea kampuni tano ambazo zinatafuta fursa za uwekezaji kwenye eneo la viwanda.

Alisema baadhi yao pia wameonyesha nia ya kuwekeza katika vifaa tiba na dawa, utengenezaji wa kuunganisha vifaa vya kilimo.

# Lukuvi atangaza eneo mgogoro kuwa makazi

**Na Munir Shemweta,**
DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ametangaza eneo lenye mgogoro wa muda mrefu la Mtakuja kata ya Chang'ombe mkoani Dodoma kuwa la makazi.

Kutokana na uamuzi huo, ameagiza kuanza kazi ya urasimishaji itakayookoa takriban Sh. bilioni 8.5 zilizokuwa zitumike kufanyiwa maboresho.

Eneo la Mtakuja, awali lilipangwa kuwa la ukanda wa kijani na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) kwa ajili ya kutunza mazingira na baadaye kupangwa kwa matumizi ya makuburi, hivyo kuingia katika mgogoro na wananchi.

Lukuvi alisema jana kuwa kutokana na uamuzi wa kulitangaza eneo hilo kurasimishwa, sasa litapimwa na kupangwa upya na hakuna mwananchi atakayevunjiwa nyumba na kila mtu atapata haki yake.

Kwa mujibu wa Lukuvi, timu ya wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma, itaanza urasimishaji wiki ijayo na kukamilika mwishoni mwa Februari, mwakani kwa wananchi kupatiwa hati za umiliki.

"Urasimishaji utakaofanyika utafuta maendelezo ya kila mwenye eneo bila kubomoa nyumba ya mtu. Tunataka kila mwananchi apate haki yake na awe na uhakika wa makazi yake ya kuishi," alisema Lukuvi

Waziri alisema kila mwananchi katika eneo la Mtakuja atalazimika kugharamia upimaji mpaka umilikishwaji na kodi za kisheria na kusisitiza kuwa anaamini hakuna mwananchi atakayeshindwa kulipia.

Lukuvi alibainisha kuwa kwa wale waliopewa maeneo lakini hawakujitokeza wakati wa uhakiki, utambuzi utaendelea ili kila mmoja apate haki yake. Wananchi 867 wamehakikiwa kati ya 1,049 hivyo kufanya wananchi 182 kuwa pekee wasiohakikiwa.

Kutokana na uamuzi wa kutangaza Mtakuja kurasimishwa, sasa hati zote za wamiliki wa ardhi katika eneo hilo zimefutwa. Eneo hilo lilikuwa na hati 65 zilizokuwa zimetolewa kwa baadhi ya wananchi.

Waziri pia alitangaza pia kufanyika uhakiki upya katika maeneo ya wananchi waliopitiwa na barabara za mzunguko katika eneo la Mtakuja ambapo awali uhakiki ulifanywa na Wakala wa Barabara (TANROADS).

Kwa mujibu wa Lukuvi lengo la kufanya uhakiki upya ni kubaini udanganyifu uliofanywa na baadhi ya wananchi wasio waaminifu waliokuwa na lengo la kujipatia kiasi kikubwa cha fedha ya fidia.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alilitaka jiji la Dodoma kuhakikisha maeneo yenye maboresho yanafanyika kwa kasi ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea kama ilivyokuwa kwenye eneo la Mtakuja alilolielezea madhara yake yametokana na uzembe wa kutofanya maboresho mapema.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Lindi, Maimuna Pasani, akizungumza kwenye kikao cha baraza Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Wilaya ya Nachingwea, katika ziara yake ya kukutana na wajumbe wa mabaraza ya umoja huo ya wilaya zote za mkoa huo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Wahamiaji haramu 15,000 wakamatwa

**Na Christina Mwakangale**

IDARA ya Uhamiaji imesema kwa kipindi cha Januari hadi Novemba, mwaka huu, imewakamata zaidi ya wahamiaji haramu 15,000 kati yao 400 wakitokea Ethiopia.

Aidha, imesema Watanzania 45 waliojihusisha na usafirishaji wa wahamiaji haramu, walikamatwa na kufikishwa mahakamani katika kipindi hicho.

Msemaji Muu wa Idara ya Uhamiaji, Mrakibu Paul Masele, aliyasema hayo jana katika kituo kimoja cha redio wakati akizungumzia Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Uhamiaji inayoadhimishwa Desemba 18, kila mwaka.

"Kuanzia Oktoba hadi Novemba, mwaka huu, tulikamata wahamiaji haramu kutoka Ethiopia zaidi ya 400 na walifikishwa mahakamani na kuhukumiwa.

Katika usafirishaji huo wa wahamiaji haramu wapo Watanzania wachache wanajihusisha na vitendo hivyo. Januari hadi Novemba, mwaka huu, tulikamata Watanzania 45 na walichukuliwa hatua za kisheria," alisema.

Pia alisema Januari hadi Novemba, walikamatwa zaidi ya wahamiaji haramu na 15,000 wamechukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria.

Alisema majukumu ya uhamiaji yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria kudhibiti, uingiaji, ukaaji na uondokaji wa watu nchini kutoa pasipoti na hati tofauti za kusafiria.

Mrakibu huyo alisema pia idara hiyo inaratibu maombi ya uraia kwa watu kutoka mataifa mbalimbali.

Kadhalika, alitoa wito kwa wananchi kutofanya biashara ya kusafirisha wahamiaji hao, kuwahifadhi na kwamba wamiliki wa vyombo vya usafiri waepuke kuwasafirisha.

Umoja wa Mataifa (UN) unasema idadi ya wahamiaji duniani kote, imeongezeka kwa asilimia 49 hadi kufikia milioni 258 kati ya mwaka 2000 na 2017.

Takwimu za Shirika la Uhamiaji wa Kimataifa (IOM) kutoka kwa mujibu wa 'Global Migration Data Analysis Center' (GMDAC), idadi ya wahamiaji ilikuwa milioni 173 mwaka 2000 na ilifikia milioni 191 mwaka 2005, huku mwaka 2010 ikiwa milioni 222.

# TBA yawabana wadaiwa sugu

**Na halfani Chusi**

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Majengo (TBA), Daud Kondoro, amewataka wadaiwa sugu wote wa wakala huo kulipa madeni yao kabla ya Januari mwakani.

Amesema wakala hautamvumilia yeyote atakayekaidi agizo hilo ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani.

Kondoro alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salam alipoongea na waandishi wa habari kuhusu hatua zinazochukuliwa na TBA kudai madeni hayo.

Alisema wakala huo umepanga kutumia njia mbalimbali katika kudai madeni kwa wadaiwa sugu ikiwamo kuwaondoa kwa nguvu kwenye nyumba kwa kutumia madalali wa mahakama ambao ndio wamepewa zabuni hiyo kwa niaba ya wakala.

"Lakini, hatua nyingine ni kuwafungulia kesi za madai mahakamani wadaiwa hao watakaokuwa wameondolewa ili kuhakikisha wanalipa madeni hayo licha ya kuwa watakuwa wameshaondolewa tayari kwenye nyumba," alionya.

Aliongeza kuwa kitendo cha wapangaji kutolipa kodi kwa wakati kimekuwa kikwazo kwenye mikakati ya TBA kutekeleza mipango yake ikiwamo ukarabati wa nyumba zilizopo pamoja na ujenzi wa nyumba mpya ambazo zitapangishwa au kuuzwa kwa watumishi wa umma.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Miliki, Said Mndeme, alisema jumla ya wadaiwa sugu 423 wameshapewa taarifa za madai yao na wakishindwa kulipa mapema, wataondolewa kama ratiba ilivyopangwa.

Aliongeza kuwa serikali imeshatoa kiasi cha Sh. bilioni 12 kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za umma katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma pamoja na nyumba zingine za wakala huo nchini.




Mkuu wa Bidhaa na Bei wa Zantel, Aneth Muga akionesha namna ya kufanya malipo kidogo kidogo kupitia akaunti ya Ezypesa ili kununua simu aina ya Smarta wakati wa hafla ya uzinduzi wa kampeni ijulikanayo kama 'Haba na Haba Hununua Smarta'. Kushoto ni Mkuu wa Zantel-Zanzibar, Mohammed Mussa.

# Wateja Zantel wawezeshwa kumiliki simu janja za Smarta

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WATEJA wa simu za mkononi za Zantel, wanaweza kununua simu aina ya Smarta kwa kulipa kidogo kidogo kuanzia Sh. 1,000 ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kampuni kuwawezesha watu wengi zaidi kunufaika na huduma za kidigitali.

Huduma hiyo imezinduliwa chini ya kampeni ijulikanayo kama 'Haba na Haba Hununua Smarta' na itawawezesha wateja wa Zantel kutunza fedha kidogo kidogo kwenye akaunti za Ezypesa na pale mteja anapofikisha kiwango cha Sh. 39,999 atakitumia kununua simu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo jana, Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohammed Mussa, alisema ikiwa kampuni ya kidigitali, imeona kuna haja ya kuja na suluhisho litakalowawezesha wateja kumiliki simu janja bila kuathiri bajeti au matumizi muhimu kwa kulipa kidogo kidogo.

"Tunatambua kwamba si watu wote wana uwezo wa kununua simu kwa kulipa pesa taslimu ndiyo maana tumekuja na huduma hii ili kuwawezesha wateja kulipa kidogo kidogo na kuwapunguzia mzigo wa kulipa kwa mara moja," alisema.

Mkuu wa Bidhaa na Bei wa Zantel, Aneth Muga, alisema mbali na kutunza pesa kwa njia ya Ezypesa, kupitia huduma hiyo, wateja wanaweza kuchangiana kwa kuingiziana kiasi cha fedha kwenye akaunti yake ya Ezypesa ili kumwezesha mmoja kumiliki simu janja aina ya Smarta.

"Azma yetu ni kuhakikisha kila mtu anafikiwa na huduma za kidigitali na anufaike na fursa zake ikiwamo kujumuika na ndugu, jamaa na marafiki lakini pia kufanya shughuli za uchumi. Kupitia huduma hii, tumerahisisha zaidi upatikanaji wa simu janja bila kujali kipato cha mteja wetu," alisema Muga.

# Bil. 38/- kupunguza vifo saratani miaka 4

**Na Romana Mallya**

SHILINGI bilioni 38 ziatatumika katika mradi wa kabambe wa kupunguza mzigo mkubwa wa matibabu na vifo vitokanavyo na saratani Tanzania (TCCP) kwa kipindi cha miaka minne.

Mkurugenzi wa mradi huo, Dk. Harrison Chuwa, alisema juzi kuwa mradi huo unatekelezwa katika wilaya 13 za mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza.

Alisema hayo ikiwa ni siku kadhaa tangu Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) na Taasisi ya Aga Khan (AKFT) wakishuhudiwa na serikali wakisaini mkataba wa makubaliano wa kutekeleza mradi huo.

Dk. Chuwa alisema mradi huo umefadhiliwa kwa ushirikiano wa pamoja kati ya AFD iliyotoa Sh. bilioni 29 na AKFT Sh. bilioni tisa.

Alisema mradi huo unaongozwa na AKFT, kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aga Khan (AKU), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI) na Hospitali ya Kitaifa ya Muhimbili (MNH).

Wengine ni Kituo cha Matibabu cha Bugando (BMC), Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

"Mradi huu unakusudia kushughulikia matatizo wakati wote wa matibabu endelevu ya saratani kwa kutekeleza ushirikiano wa ubunifu ambao unakusudia kuimarisha na kupanua ubora na upatikanaji wa huduma za saratani Tanzania," alisema.

Alitaja malengo manne ya mradi huo ni kuboresha na kupanua miundombinu iliyopo, kujenga uwezo wa wafanyakazi wa taasisi zinazoshiriki, kuimarisha uelewa wa ugonjwa huo kwa jamii na kuanzisha mikakati ya utafiti ya pamoja.

Kwa mujibu wa Chuwa, ushirikiano huo wa kipekee utawanufaisha moja kwa moja watu milioni 1.7 na utafanya kazi katika vituo vya afya 100 katika ngazi zote kwenye mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza.



# COSTECH yatoa mil. 297/- kuboresha zabibu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imetoa Sh. millioni 297 kwa ajili ya kuboresha kilimo cha zabibu katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Makutupora.

Aidha, TARI Makutupora kupitia fedha hizo, imekuwa ikitoa mafunzo ya kilimo cha Zabibu kwa wakulima wadogo mkoani hapa ili kukuza na kuboresha zao hilo. Akizungumza jana wakati wa ziara ya kutembelea kituo hicho, Mkurugenzi wa Kituo hicho, Dk. Cornel Massawe, alisema fedha hizo wametumia pia katika ujenzi wa kiwanda kidogo cha kuchakata zabibu. "COSTECH ilitupatia fedha kwa ajili ya kuboresha zao la zabibu katika kituo chetu ambazo tumekuwa tukitumia katika shughuli za kilimo cha zabibu," alisema Dk. Massawe.

Dk. Massawe alisema kiwanda hicho kinatumika kuchakata zabibu kwa ajili ya kutengeneza jiusi na mvinyo lakini pia kinatumika kutoa mafunzo kwa wakulima na wafanyabiashara wa bidhaa hizo.

Mtafiti wa Udongo wa kituo hicho, Ashura Ally, alisema wamekuwa wakitoa mafunzo kwa wakulima hao kuanzia uandaaji wa mashamba hadi uvunaji.

Alisema wakati wa kuandaa shamba la zabibu, mtu ni lazima aangalie udongo, shamba liwe safi, kupanda miche kwa mpangilio na kuzingatia vipimo vya mbolea na udongo.

"TARI tuko hapa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima, hivyo tunapenda kuwakaribisha wakulima wote wanaohitaji kujifunza kwa makundi na mtu mmoja anakaribishwa," alisema Ally.

Naye Mtafiti katika Idara ya Uhawilishaji na Usambazaji wa Teknolojia TARI Makutupola, Stella Hambangabe, alisema Dodoma ni sehemu pekee katika kilimo cha zabibu ambako kinafanyika kwa misimu miwili.

"Zao la zabibu ni fahari ya Dodoma kwani hali ya hewa ya hapa inakuza kilimo cha zabibu, hivyo ni vyema kila mmoja ajikite kuendesha kilimo hicho," alisema.

Mtafiti huyo alisema kituoni hapo wanatoa mafunzo ya utunzaji na upandaji wa mazao mengine kama mihogo na korosho.

Hambangabe alisema hadi sasa wamewafikia wakulima 3,500 wa mkoani hapa ambao wamenufaika na elimu ya kilimo hicho




Baadhi ya wahitimu wa mahafali ya 11 ya Chuo Kikuu cha Dodoma, (UDOM), wakiwa ndani ya ukumbi wa Chimwaga Chuoni hapo jana, Jijini Dodoma, kwenye mahafali hayo, jumla ya wahitimu 8206 walitunukiwa shahada mbalimbali ikiwamo uzamivu, uzamili na shahada ya kawaida.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kanisa laandaa hafla Watanzania kupenda, kutumia bidhaa za ndani

**Na Peter Mkwavila,**
CHAMWINO

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya uzinduzi wa ibada maalumu itakayofanyika katika kanisa la Kristo Mfalme Anglikana Chamwino kwa ajili ya kuwahamasisha Watanzania kuzipenda bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, Mratibu wa tukio hilo, Simon Gunju, alisema ibada hiyo malengo yake ni kuwahamasisha Watanzania kuzipenda bidhaa zinazozalishwa nchini ili kuimarisha uchumi wa taifa na kukuza ajira.

Gunju alisema mbali na Spika, viongozi wengine wanaotarajiwa kuwapo ni Askofu Mkuu Mstaafu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Dk. Donard Mtetemela, wanasiasa, mawaziri na wabunge.

Mratibu huyo pia alisema lengo lingine ni kuwajengea uwezo wa elimu ya uzalendo ya kuona umuhimu wa kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini badala ya zinazotoka nje ya nchi.

Alisema lengo kuu pia ni kuona nchi ya Tanzania inazalisha bidhaa zake yenyewe na Watanzania wazipende na kuthamini ili kukuza uchumi na ajira kwa Watanzania wenyewe.

"Tatizo kubwa lililopo kwa Watanzania walio wengi ni elimu yao imekuwa ndogo ya kuelimisha na kuvipenda vitu vyao zaidi, tofauti na elimu waliyojijengea ya kuzipenda bidhaa zinazotoka nje wakati hivi sasa nchi yetu ina bidhaa zenye thamani kubwa tena ni bora zaidi," alisema.

Alisema pamoja na kusisitiza Watanzania kupenda bidhaa zao zinazozalishwa hapa nchini, pia serikali itahamasishwa kuhakikisha viwanda vyake vinakuwa bora kwa uzalishaji ili bidhaa za viwanda hivyo zipendwe na kutumika.

# Taasisi binafsi zasifiwa elimu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKURUGENZI wa Elimu Maalum Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Julius Migeha, amesema serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na taasisi za kiraia zikiwemo za kidini katika kusaidia elimu jumuishi kwa watoto wenye uhitaji maalum.

Migeha aliyasema hayo jana alipokuwa akiwasilisha mada juu ya umuhimu wa kuimarisha mfumo wa elimu jumuishi shuleni kwenye kongamano la wadau tasnia hiyo.

Alisema serikali inaheshimu na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na wadau wa taasisi za kiraia na zile za kidini katika kuhakikisha vipaumbele vyote vilivyowekwa vya utekelezaji kwa ajili ya shule zenye watoto wenye ulemavu inatekelezeka bila kipingamizi.

Kwa mujibu wa Migeha, jitihada hizo ni pamoja na serikali kuhakikisha walimu wote wenye sifa na taaluma wanaajiriwa huku kwa upande wa vifaa visaidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu vinapatika kwa kushirikiana pande zote mbili.

Pia alisema juhudi kubwa za kuboresha miundombinu zinafanyika kwenye majengo ya shule zote ikiwa ni sehemu ya ushirikiano kati ya wadau hao wa elimu na serikali.

Hata hivyo, alisema kuwa serikali pia imejipanga kuimalisha uchunguzi na ubainishaji wa watoto wenye mahitaji maalum, ili wapatiwe unafuu stahiki hii ni pamoja na kuboresha mafunzo kazini kwa walimu wa elimu maalum.

Mkurugenzi huyo pia aliwataka wazazi na walezi wenye watoto ambao wana ulemavu wanaosoma kuwa na tabia ya kuweka bajeti kwa ajili ya kuwasomesha huku wakihakikisha wanafika shuleni na kupata elimu.

Mratibu wa Mradi wa Elimu Jumuishi Dodoma Jiji na wilaya ya Bahi, Jane Mgidange, aliwaomba wazazi wenye watoto walemavu kushirikiana na serikali na wadau mbalimbali wa elimu ili wale wanaowaficha waweze kuacha vitendo hivyo kwa kuwa ni vya ukatili na unyanyasaji.

Alisema bado kuna baadhi ya wazazi na walezi wanaendelea kuwaficha watoto ambao kama wakitolewa na kupatiwa elimu au ufundi wangeweza kuwa msaada mkubwa katika kujikwamua kwenye umasikini.



# ZEC yataja tarehe ya uchaguzi mdogo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imesema itaendesha uchaguzi mdogo wa uwakilishi jimbo la Pandani, Pemba na udiwani katika wadi ya Kinuni, Unguja Machi 28, mwakani.

Uchaguzi huo mdogo unatarajia kufanyika ili kuziba nafasi zilizowazi baada ya wateule wa uwakilishi na udiwani kufariki dunia.

Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Mabruki Jabu Makame, alisema katika uchaguzi huo mdogo hakutakua na kura ya mapema.

"Ifahamike kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi namba 4 ya mwaka 2018, upigaji wa kura ya mapema utatumika katika uchaguzi mkuu au uchaguzi mdogo wa urais pekee. Kwa hivyo, uchaguzi mdogo wa uwakilishi Pandani na udiwani Wadi ya Kinuni, hautakuwa na upigaji wa kura ya mapema," alisema.

Akitoa ratiba ya uchaguzi alisema Machi 3 hadi 11 ni uchukuaji na urejeshaji wa fomu kwa nafasi hizo, Machi 12 uteuzi wa wagombea na Machi 12 hadi 26 ni kampeni.

Pia alisema ZEC inaendelea na majukumu yake baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, imepokea taarifa za kuwapo kwa nafasi za wazi za viongozi wateule ambao wamefariki dunia. "Novemba 18, Tume ilipokea taarifa kutoka kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi ya kuwapo wazi nafasi ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Pandani kutokana na kifo cha aliyekuwa mwakilishi mteule wa jimbo hilo kupitia chama cha ACT Wazalendo, Abubakar Khamis Bakari, kilichotokea Novemba 11," alisema.

Alisema tume pia ilipokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa ya kuwapo kwa nafasi ya wazi ya kiti cha udiwani katika Wadi ya Kinuni kutokana na kifo cha aliyekuwa diwani wake, Suleiman Hassan Mohammed, kilichotokea Novemba 9," mwaka huu.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na watendaji wa serikali na kamati za ulinzi na usalama Pemba akiwa katika ziara ya kikazi jana. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi asema amegundua ufisadi katika kipindi kifupi cha uongozi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi, amesema katika kipindi kifupi cha uongozi wake, amegundua ufisadi mkubwa ndani ya serikali na taasisi zake, hivyo kuahidi kuchukua hatua.

Kutokana na hali hiyo, amewaomba wananchi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumvumilia anapochukua uamuzi mgumu ili fedha za umma ziheshimiwe na kutokomeza rushwa na ufisadi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi katika ukumbi wa Fidel Castro, Chake Chake, Pemba, alipokuwa akitoa shukrani kwa viongozi wa CCM, jumuiya zake, na Wazee na mabalozi wa chama hicho.

Alisema katika maendeleo hatakuwa na muhali na hatamwonea mtu yeyote haya na kubainisha kuwa kila unayemgusa katika ubadhirifu ni mtoto au jamaa wa kiongozi fulani. "Nivumilieni nichukue maamuzi (uamuzi) magumu (mgumu) lakini nataka niwahakikishieni kuwa baada ya maamuzi nitakayoyafanya kila senti ya fedha zetu itaheshimiwa," alisema Dk. Mwinyi.

Aliwaeleza viongozi hao kwamba katika uongozi wake fedha atakazotafuta hatakubali kuchezewa hata kidogo na amegombea nafasi hiyo ya urais kwa lengo la kuwatumikia wananchi. Katika kutekeleza aliyowaahidi, alisema ni vyema viongozi hao kuwa tayari kwa yale yote watakayoyasikia katika kipindi hiki.

Alisema katika kipindi hiki cha kwanza katika uongozi wake lazima achukua uamuzi mgumu na hana lengo la kutafuta mchawi na wala kufukua makaburi.

Pia alisema miradi yote mikubwa iliyotekelezwa ikiwamo Maendeleo ya Miji (ZUSP) ambao umegharibu Dola za Kimarekani milioni 93, miradi ya maji na miradi mengine imetumia fedha nyingi lakini matokeo yake hayaridhishi, hivyo ni lazima hatua zichukuliwe.

Aliahidi kuisimamia miradi hiyo ili kupata thamani ya matumizi ya fedha zilizotumika ambazo ni nyingi na kueleza kwamba katika hatua hiyo wapo watu watakaoguswa.

Dk. Mwinyi aliwaeleza viongozi hao pamoja na wananchi kwamba ahadi alizozitoa katika kipindi cha kampeni, zitatekelezwa kwa ustadi mkubwa.

Aliwapongeza viongozi wote wa CCM kisiwani humo kwa ushindi wa kishindo uliopatikana na chama hicho kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na viongozi hao, wanachama pamoja na wananchi.

Kadhalika, aliwapongeza viongozi wa dini zote kwa kuhubiri amani wakati wote wa uchaguzi na kusababisha mchakato huo kwenda vizuri na kuleta mafanikio makubwa.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdallah Juma Mabodi, aliwapongeza viongozi hao wa CCM kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuhakikisha wanakipa ushindi wa kishindo chama chao cha CCM kisiwani humo.

Viongozi hao wa CCM walieleza kuwa ushindi uliopatikana mwaka huu katika uchaguzi mkuu ni wa kihistoria hasa katika Mkoa wao wa Kusini Pemba ambapo CCM imepata ushindi wa wadi zote 19, wabunge majimbo tisa uwakilishi na ubunge majimbo saba pamoja na kupata nafasi zingine zikiwamo za viti maalum.

# Viongozi SMZ vyombo visivyo na bima kukiona

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameagiza chombo chochote cha moto cha usafiri kiwe cha binafsi au cha serikali kuwa na bima kuanzia sasa. Amesema endapo chombo cha serikali kitapata ajali, atakayewajibika kulipa hasara itakayotokea ni mkuu wa taasisi inayotumia chombo hicho wakimwamo mawaziri, makatibu wakuu, wakurugenzi na wakuu wa taasisi za umma.

Hemed aliyasema hayo jana ofisini kwake Vuga, Mjini Zanzibar, wakati akizungumza na uongozi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ulioambatana na wakurugenzi na mameneja wa mashirika ya bima nchini.

Alisema sheria tayari imeshalekeza vyombo vyote vya moto lazima vikatiwe bima lakini inasikitisha kuona bajeti za vyombo hivyo kwa taasisi za umma imekuwa ikitengwa kila mwaka lakini hakuna mfumo sahihi wa fedha unaotumiwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Hemed aliwataka viongozi wa taasisi zote kuhakikisha wanasimamia vyema upatikanaji wa mapato ya serikali na kuepuka rushwa, ubadhirifu, uzembe na ukosefu wa uwajibikaji ambao serikali imejitolea kupambana nao kwa hali yoyote ile. Makamu wa pili huyo alisema sekta ya bima imekuwa na mchango mkubwa wa kuongeza mapato ya taifa na kwamba Serikali ya Zanzibar imedhamiria kuweka mkazo zaidi katika eneo hilo muhimu la fedha. Akizungumzia mawakala wababaishaji, Hemed alimtaka Kamishna wa TIRA kufuatilia taasisi zinazojihusisha na mawakala wa aina hiyo na atakapogundua, lazima achukuwe hatua za kisheria mara moja.

Alisema mawakala wababaishaji wanapaswa kuondolewa mara moja kutokana na dhuluma wanayoifanya katika jamii kwa vile haikubaliki hasa ikizingatiwa kwamba inarejesha nyuma imani ya wananchi wanaohitaji huduma za bima. Hemed aliushauri uongozi wa mamlaka hiyo kuimarisha ofisi yake pamoja na kuongeza wanasheria Visiwani Zanzibar watakaowajibika kuondosha changamoto zinazowakuta wananchi hasa kwenye kesi za madai ya vyombo vinavyopata ajali ambazo huchukuwa muda mrefu." Zipo kesi za masuala ya bima hasa ajali zinazoshindwa kupata ufumbuzi kwa kukosa Mwanasheria. urasimu lazima uondoshwe kwa vile serikali haipendelei kupata au kusikia malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya suala hilo," alisisitiza Hemed.

Kamishna wa TIRA, Dk. Musa Juma, alisema washirika wa bima ndio wenye jumuku la kusimamia mapato sahihi ya taifa na kwamba iko mikakati tofauti inayotekelezwa kwa lengo la kuwafikia wananchi ambao ndio wadau wakuu.

Hata hivyo, alisema safari ya kuelekea kwenye soko sahihi la bima bado ni ndefu kutokana na uelewa mdogo wa wananchi walio wengi hasa katika masuala ya kuweka bima kwenye matukio ya majanga pamoja na ajali zinazosababishwa na vyombo wanavyotumia.



# MZEE JENGUA
# Ameondoka akiwa na mengi moyoni...

WIKI hii tasnia ya filamu nchini imeondokewa na mwigizaji mkongwe, Mohamed Fungafunga, maarufu kama Mzee Jengua, ambaye amefariki dunia Desemba 15, mwaka huu na kuzikwa katika makaburi ya Mburahati jijini Dar es Salaam.

Kifo chake kimeleta mshtuko kwa watu wengi, ambao wanajiuliza msanii huyo maarufu alikuwa akiumwa nini na kwa nini hakuna aliyejua kwamba mzee Jengua ni mgonjwa.

Maswali hayo, hayawezi kuondoa uhalisia kwamba bingwa huyo katika sanaa ametuacha na amekwenda zake mbele za haki.

Kifo chake kimeibua tena kile ambacho marehemu alichokuwa akikiita unafiki wa wasanii wa filamu nchini, ambao hupenda kujipendekeza katika misiba, lakini wanakimbia pale mmoja wao anapofikwa na matatizo.

Moja ya video yake fupi ambayo imesambaa katika mitandao ya kijamii, Mzee Jengua, ameonekana akikemea tabia hiyo kukimbia matatizo na kuita ya kinafiki na yenye kuonyesha picha mbaya katika jamii inayowatazama.

Kile alichokisema ni kama alikuwa akijitabiria, kwani wakati wa ugonjwa wake hakuna msanii aliyejitokeza kumsaidia, badala yake walijitokeza msibani na kila mmoja akisema alikuwa hajui kama alikuwa akiumwa.

Wakati akiumwa hakuna msanii aliyejitokeza kumsaidia, na hata alipoamua kwenda kuugulia kwa mtoto wake Mkuranga, hakuna aliyekwenda kumjulia hali.

Ukweli ni kwamba Mzee Jengua, amekufa alikuwa akijua udhaifu wa wasanii wenzake na ndio maana aliamua kutema nyongo mapema, angalau aende akiwa hana dukuduku moyoni.




BASI SAWA

## Kingwendu hilo sijui kama litawezekana

MCHEKESHAJI, Kingwendu, ameiomba serikali iwaangalie wasanii kwa kuwapatia madaktari wa kuchunguza afya zao mara kwa mara.

Kingwendu amesema suala hilo litakuwa zuri ili wasanii wanapoumwa wajue kabisa ni ugonjwa gani ambao unamsumbua na kuepusha utata unaotokeaga kuhusu chanzo cha kifo.



"Fundisho kubwa kwa wasanii kama unaumwa usilazimishe kufanya kazi jaribu kufuatilia vipimo hospitalini ili kuangalia afya zetu, pia tungejaribu kuongea na Serikali ituangalie na tuwe na madaktari wetu wa kutufanyia 'check up' ili mtu anapoumwa ijulikane anaumwa nini" amesema.

## Ramso High atambulisha 'Vibweka'

MWANAMUZIKI chipukizi, Ramadhali Idd, maarufu kama 'Ramso High' ametambulisha video ya ngoma yake mpya inayoitwa 'Vibweka'.

Ramso High amesema video ya wimbo wake huo imeanza kurushwa katika vituo mbalimbali vya Televisheni na radio, pia unapatikana katika mtandao wa You Tube.



"Vibweka unaelezea namna ya watu wasivyojali na kuthamini wapenzi wao, nia yangu kutoa fundisho watu kuheshimiana na kumthamini mwenza wako," amesema Ramso High.

Wimbo huo utakuwa wa tatu kwa mwanamuziki huyo, ikiwamo Dhuluma na Nalewa ambayo inaendelea kufanya vizuri.



## Bajeti ya mbwa wa Wema Sepetu usipime

MWIGIZAJI staa wa Bongo Muvi, Wema Sepetu, ameibua mjadala mzito katika mitandao ya kijamii, baada ya kueleza huwa anampeleka saluni mbwa wake aitwaye Vanilla Nunu.

Wema ameweka posti yake katika mtandao wa Istagram, akisema mbwa wake huyo jike, anampeleka saluni mara mbili kwa mwezi kwa ajili ya kumrembesha.

"Mtoto wangu amefurahia siku yake ya saluni leo, ndiyo huwa anaenda saluni mara mbili kwa mwezi"

Baada ya kuweka posti hiyo ikiambatana na picha ya mbwa huyo ambaye ana wafuasi zaidi ya 10,000 kwenye mtandao huo, mashabiki wake walianza kutoa maneno ambayo yalionekana wameshtuka kusikia mbwa huyo anahudumiwa kama binadamu..



## Video 'Giny Baba' sasa hadharani

HATIMAYE mwanamuziki wa Bongo Fleva anayekuja kwa kasi, Joshen Adam, maarufu kama Giny, amekamilisha video ya wimbo wake mpya inaojulikana kama 'Giny Baba'.

Akizungumza na BT, Meneja wa mwanamuziki huyo, Yasin Said, anayejulikana kama Yaso Boy, amesema video hiyo ambayo imetengenezwa na Blue Image chini ya muongozaji Ibrasoo, itazinduliwa hivi karibuni.

"Video ya ngoma yetu mpya imekamilika, kuanzia Jumatatu itaanza kuruka hewani katika vituo vya televisheni, lakini watu wanaweza kuitazama kupitia mtandao wa You Tube kwa jina la Giny Baba," amesema.

Amewataka mashabiki wa muziki kumuunga mkono mwanamuziki huyo ambaye ameamua kuleta ladha katika muziki wa kizazi kipya hapa nchini.

## ZILIPENDWA ZINAZOPENDWA HARUSINI

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA hali ya kushangaza, nyimbo za muziki wa dansi hasa zile za miaka ya nyuma zimeonekana kupendwa zaidi kadili miaka inavyozidi kusonga mbele.

Ni tofauti na muziki wa kisasa, bongo fleva ambayo kila miaka inavyozidi kusonga mbele, inasahaulika na huisikii tena. Na hata ikitokea kwa bahati ikisikika hakuna mtu mwenye mzuka nayo tena. Kila mtu anataka asikie nyimbo mpya tu za bongo fleva.

Lakini nyimbo za muziki wa dansi kuanzia miaka ya 1970, hadi mwanzoni mwa 2000, zikipigwa leo unaweza ukadhani labda ni wimbo mpya. Kitakachokujulisha kuwa si nyimbo mpya ni pale utakapoona kila mmoja anauimba.

Imekuwa ni kawaida sasa kwenye sherehe za harusi maeneo mbalimbali nchini, pamoja na nyimbo nyingine za kisasa, lakini kuna baadhi ya nyimbo za zamani huwa hazikosekani.

Leo tunaziangalia nyimbo za dansi zinazopedwa na marika yote, na hupendwa kupigwa hasa kwenye sherehe za harusi na laba kuwapo na watu wachache wanaobaki kwenye viti kama hakuna kabisa.

**Kuoana ni Jambo la Sifa-Afro 70 Band**

'Kuoana' uliopigwa na Afri 70 Band, utunzi wake marehemu Patrick Balisidya.

Ni wimbo waliotunga na kuutoa katikati ya miaka ya 1970, kwenye harusi ya dada yake Ndyanao Balisidya. Ikumbukwe Nyandao aliondokea kuwa mkufunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mtafiti na mtunzi na vitabu maarufu vilivyosomwa kwenye shule mbalimbali nchini Tanzania.

Wimbo huu umekuwa alama ya harusi mbalimbali nchini, kwani maneno yake hayamlazimishi mzazi kuongea, bali maudhui peke yake ni mafundisho tosha.

**Kitambaa Cheupe-King Kiki**

Wengi hudhani kuwa wimbo huu ilitungwa na kurekodiwa labda miaka ya 1970. Wimbo huu ulirekodiwa mwanzoni mwa miaka ya 2000. Lakini kwa sababu ni wa dansi na umeimbwa na mwanamuziki mkongwe, Kikumbi Mwanza Mpango 'King Kiki', basi wengi huuona ni wa zamani.

Huu nao ni moja kati ya nyimbo ambazo hazikosekani kwenye sherehe za harusi na kuwachengua watu vilivyo.

**Georgina-Marijani Rajab**

Kwa bahati mbaya sana, Georgina aliyeimbwa kwenye wimbo huu, alifariki mwishoni mwa mwaka jana, au mwanzoni mwa mwaka huu. Wakati huo alikuwa msichana mrembo, wakati akiimbwa na bendi ya Dar International.

Aliyetunga wimbo huu ni Khalfan Uvuruge, lakini ukaimbwa na Marijani Rajab kwa ufundi wa hali ya juu katikati ya miaka ya 1970.

Hakuna kijana yoyote wa kizazi cha sasa ambaye haujui wimbo huu. Kwenye harusi ndiyo usiseme, lazima upigwe.

**Rangi ya Chungwa-Nyanyembe Jazz**

Umepigwa na bendi ndogo tu wakati huo, inaitwa Nyanyembe Jazz ya mjini Tabora, lakini hadi leo umekuwa ni wimbo maarufu zaidi. Ukitafuta nyimbo 10 bora za dansi, bongo fleva, hip hop, huu haukosi. Na harusi yoyote haiwezi kwisha kama wimbo huu bado haijapigwa.

**Masafa Marefu-Tancut Almasi**

Moja kati ya wimbo uliokuja juu kwa sasa kwa kupendwa kwenye mahasuri ni huu wa 'Masafa Marefu.'

Cha ajabu umekuwa ukiombwa hata na vijana wadogo, na ukipigwa basi hata kabla watu wazima hawajaanza kucheza, wao tayari wanakuwa wameshaanza kulisakata rhumba.

Ulipigwa na bendi ya 'Tancut Almasi' kutoka mkoani Iringa.




## Ndoa ya Msukule: Ngoma inayochezwa na wasiyoijua

**Na Adam Fungamwango**

DUNIANI kuna mambo ya ajabu sana. Mengine unaweza kudhani ni ya kufikirika, lakini unaambiwa yapo na yanatendeka kwenye dunia hii ya Mungu.

Kuna hii dhana ya misukule. Inadaiwa kuna baadhi ya binadamu wanawafanyia wenzao uchawi au mazingara, ili kwa hali ya kawaida waonekane kuwa wamekufa, lakini ukweli ni kwamba wapo hai.

Inadaiwa kuwa kinachokwenda kuzikwa ni mgomba tu, lakini binadamu mwenyewe anakuwa yupo hai, na anakwenda kutumiwa kwenye kazi mbalimbali na aliyemfanya hivyo, kama vile kulima, kufanya kazi ngumu, kumtumikisha kwa kitu chochote kile, au hata kumtumikisha kingono.

Dhana hii ndiyo imemfanya mtunzi kwa filamu hii kutunga kisa kinachohusiana na hayo.

Filamu inaitwa 'Ndoa ya Msukule'. Imechezwa na msanii maarufu nchini Fadhili Msisiri, maarufu kama mzee Msisiri wa Msisiri. Wengine ni Kanywele Fumbo, Mary Alex, Joshua Mnubi, Martha Martin na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa mzee Msisiri anampenda msichana mmoja aitwaye Wispa Michael.

Mzee Msisiri anamwambia kabisa kuwa anataka kumuoa na si kuwa mpenzi wake tu.

Msichana anakataa kwa sababu tayari ana mchumba wake anaitwa Mussa.

Kuona hivyo mzee Msisiri anaamua kutumia



nguvu za ziada. Anafanya uchawi ili ampate Wispa.

Siku chache baadaye msichana anagongwa na gari. Msiba unahuzunisha wengi, anazikwa na maisha yanaendelea.

Nyuma ya pazia ni kwamba mzee Msisiri alimchukua kama msukule. Wispa hakufa, ila alichukuliwa kimazingara kwa lengo tu la kutaka awe mke wake, lakini kwa kiswahili kizuri ni kwamba amtumikishe kingono kwa sababu hakukuwa na makubaliano yoyote na ndoa haijafungwa. Baada ya mwaka mmoja, mzee Msisiri anafariki na watoto zake anaiuza nyumba ya baba yao.

Kumbe baba yao ndani alikuwa anaishi na msukule wa Wispa. Walioinunua wanaanza kuipangisha.

Inakuwa ni kizaazaa tu, kila mpangaji anayoingia, anakutana na mauzauza kibao.

Ikafikia wakati watu wakawa hawapangi tena kwenye nyuma ile, na walikuwa wakipanga ni watu wanaotoka mbali na pale.

Mwisho wa siku mchumba wa 'marehemu' Wispa, Mussa alikwenda kupanga kwenye nyumba ile.

Mauzauza yaliendelea, lakini yalikuwa kinyume chake. Badala ya vurumai na purukushani, Mussa anakwa anapikiwa chakula. Akirejea anakuta chai mezani, wakati mwingine chakula. Akawa haelewi nini kinaendelea.

Hata hivyo alipata ushauri kwenda kwa mchungaji ili kukiombea chumba kutokana na mauzauza. Mchungaji alikuja na kuomba. Kilichoonekana ni kugundulika kuwemo kwa Waspa chumbani.

Ulikuwa na mshangao kwa kila mmoja, lakini mchungaji akaeleza kuwa msichana huyo aliwekwa msukule ndani. Baada ya hapo kila kitu kikajulikana. Mussa na Waspa wakakutana tena, wazima wa afya.



# Nyota hawa hatari TikTok 2020

DESEMBA 15 mtandao wa kijamii wa TikTok, ulitoa majina ya wasanii 10 wa Nigeria waliofanya vizuri mwaka 2020 kwa video zao kupendwa na watazamaji wengi.

Kulingana na meneja operesheni wa mtandao huo, Boniswa Sidwaba, TikTok inajivunia kuwa na wasanii hao nyota kwani wamewafanya watumiaji kupata furaha.

Wasanii walioingia kwenye orodha hiyo ni Don Jazzy,

Iyabo Ojo, Mr. Macaroni, Symply Tacha, Yemi Alade.

Toke Makinwa, Tiwa Savage, Korede Bello, Official Regina na Mercy Johnson-Okojie.



## Cossy, Abel waachana rasmi

MWIGIZAJI nyota wa Nigeria, Cossy Orjiakor na mchumba wake Abel Jurgen, hatimaye wamevunja uhusiano wao baada ya kudumu kwa muda mrefu.

Wote wawili, Orjiakor na Jurgen, wanatuhumiana kusababisha kuvunjika kwa penzi lao kutokana na malalaliko ya unyanyasaji wakati wakiishi pamoja.

Mtu wa kwanza alikuwa Abel, ambaye alilalamika kuwa waigizaji wa kike wa Nollywood, wamekuwa wakimfuata mpenzi wake na kumwambia yeye huwa anamsema vibaya wakati akiwa amelewa.

## Omah hukujua Uganda wapo karantini?

WANAMUZIKI wawili wa Nigeria, Omah Lay na Tems, wamefikishwa mahakamani nchini Uganda kwa tuhuma ya kukiuka kanuni za kupambana na ugonjwa wa Covid-19

Wasanii walikamatwa wiki iliyopita baada ya kutumbuiza katika tamasha moja la usiku, jambo ambalo ni kinyume na kanuni zilizowekwa na serikali za kupambana na virusi cha Corona.

Omah aliweka ujumbe katika akaunti yake ya Twitter, akisema "Hivi sasa nipo kwenye matatizo nchini Uganda pamoja na Tems, kama mwanamuziki nilijaribu kuburudisha, sikuandaa tamasha lakini tulikamatwa na kufunguliwa mashtaka," ameandika.





## Tyler Perry hajui kama anaishi

MSANII tajiri wa filamu nchini Marekani, Tyler Perry, yupo njia panda kuhusu hatma ya maisha yake tangu kuachana na mke wake.

Akishiriki ujumbe katika mitandao ya Twitter na Facebook, staa huyo amesema bado anashangaa kutokana na kutojua juu ya maisha yake ya baadae.

"Kama najiona nipo kwenye maisha ya mpito, nina miaka 51, sina mke na nashanagazwa na ukurasa unaofuata wa maisha yangu yatakavyokuwa, sitajali kama natembea na Mungu," amesema.


## Kylie , Kanye vinara kwa mkwanja 2020

JARIDA maarufu la Forbes, limetaja majina ya mastaa ambao wanaongoza kulipwa pesa nyingi kwa mwaka 2020.

Miongoni mwa wasanii maarufu waliotajwa ni Kylie Jenner na Kanye West, ambao wanaongoza katika orodha hiyo.

Jenner alilipwa kiasi cha dola milioni 590, akifuatiwa na rapa West ambaye alilipwa milioni 170.

Kulingana na, Forbe, wanaofuatia ni Tyler Perry, ambaye amejikusanyia milioni 97, akifuatiwa na mchezaji wa NBA, Lebron James na mwigizaji Dwayne Johnson.



MAKALA

# Utafiti za wasomi zitoe majibu ya matatizo yetu

## ■ARU yaanza na teknolojia kutengeneza mkaa

Na Mwandishi Wetu

MATATIZO mengi kwenye jamii yanaweza kupata majibu kama wasomi wetu watajichimbia na kuja na majibu ya kisomi ya matatizo hayo kwa kufanya tafiti nyingi kwani hapo watakuwa wametumia elimu yao ipasavyo kuiokoa jamii.

Haitoshi tu kwa msomi kupata Shahada ya kwanza, yapili au ya Uzamivu bali kinachotakiwa ni kwa wasomi wetu kufanya tafiti mbalimbali kuhusu shida zilizopo kwenye jamii na kuja na majibu yenye ufumbuzi badala ya kila kitu kutafuta wazungu.

Vyuo vikuu ni visima vya maarifa kwani kumejaa wasomi wa ngazi mbalimbali kuanzia wenye Shahada ya Kwanza, Shahada ya Uzamili, Shahada ya Uzamivu na maprofesa wa fani mbalimbali hivyo ni eneo ambalo wakiamua kwa dhati kabisa wanaweza kuleta mabadiliko hapa nchini.

Chuo Kikuu Ardhi (ARU) kimekuwa mfano wa utekelezaji wa maono hayo kwa kufanya tafiti nyingi zenye manufaa kwa taifa na hivi karibuni kilibuni teknolojia ya kutengeneza mkaa mbadala unaotokana na taka ngumu kikisema kuwa kinalenga kuongeza ujuzi na ajira kwa wahitimu wa vyuo vikuu na wakulima wadogo.

Teknolojia hiyo inaweza kuwa mkombozi wa mazingira kwa maana ya kupunguza au kumaliza tabia ya ukataji wa miti kwaajili ya mkaa kama ambavyo imezoeleka kwenye jamii.

Kwa sasa matumizi ya mkaa yamekuwa makubwa sana kiasi cha kutishia uhai wa misitu yetu hivyo kama utafiti huu wa ARU utatiliwa maanani na kuendelezwa ni dhahiri tutaokoa misitu.

Ubunifu kama huu ni wa kuungwa mkono na kuendelezwa kwaajili ya mustakabali wa nchi kwani ni kwa muda mrefu wadau wa mazingira duniani wamekuwa wakilalamikia ukataji miti kwaajili ya mkaa kama janga linaloitesa dunia leo na kesho.

Teknolojia hiyo ni suala muhimu na ambalo serikali inapaswa kulitilia mkazo kwani litaliokoa taifa kuelekea kuwa jangwa kwani watu watahamia kwenye matumizi ya kuni mbadala na kuachana na ukataji wa miti ambayo ndiyo maisha ya sasa

Akizungumza kwenye mahafali ya 14 ya chuo hicho hivi karibuni, Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Evaristo Liwa, alisema chuo hicho pia kimefanya utafiti wa kuboresha matumizi na mbinu mpya za umwagiliaji katika bonde la mto Rufiji ili kuleta tija na kuongeza uzalishaji katika Wilaya ya Iringa pamoja na kutatua changamoto mbalimbali za matumizi ya maji katika mto Rufiji

Profesa Liwa anasema chini ya ufadhili wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), chuo kimefanya utafiti kuhusu teknolojia ya asili ya ujenzi wa nyumba zinazostahimili matetemeko ya ardhi katika mji wa Dodoma na utafiti huo utawezesha kutumia taaluma hiyo kwenye ubunifu wa majengo ya kisasa ya mkoa huo.

Utafiti kama huo unamanufaa makubwa kwa Watanzania hasa ikizingatiwa kuwa utasaidia kuwakinga watu wengi na majanga ya asili ambayo iwapo yatatokea yatasababisha uhalibifu mkubwa wa mali na wakati mwingine kugharimu maisha ya watu

Ingawa ni kwa nadra sana majanga ya asili kama matetemeko ya kiwango kikubwa kutokea kwa hapa nchini lakini ni vyema hatua kama hizo zinazochukuliwa na ARU zikaungwa mkono na kuendelezwa ili watu wakajenga kwa kuzingatia hilo hasa kwenye maeneo yenye uwezekano wa kutokea matetememo.

Nchi inapoelekea kwenye uchumi wa viwanda tafiti si jambo linalohitaji mjadala kwani ni suala muhimu linalohitaji kutiliwa mkazo na serikali, watu binafsi na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kufikia ndoto ya Tanzania ya viwanda.

Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli amekuwa akisisitiza kuipaisha Tanzania kiviwanda hivyo moja ya nguzo kuu kufikia ndoto hizo ni kufanya tafiti mbalimbali ambazo zitaweza kuwezesha ugunduzi wa teknolojia mbalimbali ambazo zinaweza kuuzwa hata nje ya nchi. Imekuwa kawaida kwa nchi mbalimbali za Afrika kuagiza au kunakili teknolojia zilizobuniwa na mataifa ya Ulaya, Marekani na Asia lakini umefika wakati wasomi wetu waonyeshe thamani ya usomi wao kwa kufanya tafiti nyingi na kugundua teknolojia.

Imekuwa kawaida kuona wataalamu wetu wakienda kwenye mataifa mbalimbali yaliyoendelea kwaajili ya kujifunza mambo mbalimbali ikiwemo teknolojia mpya lakini hatuwezi kujivunia sana hilo kwani ufike wakati na wao waje kujifunza Tanzania.

Elimu wanayopata wasomi wetu inatakiwa kuwa chachu ya kuwa wabunifu wa mambo mbalimbali ili kuwapa tamaa vijana wanaochipukia wanapoona wasomi wamebuni teknolojia mbalimbali ambazo mwishowe zinakuwa na manufaa kwa nchi.

Ndiyo sababu tafiti zinazofanywa na ARU ni muhimu kwa ustawi wa taifa na vyuo vikuu vyote ambavyo ndiyo visima vya maarifa wafanye tafiti nyingi kadri ya uwezo wao ili waje na majibu ya matatizo mengi yanayosumbua kwenye jamii yetu

Kwenye mahafali ya 14, Profesa Liwa alisema ARU imefanikiwa kuwa na matokeo ya utafiti yaliyohusu 'uhitaji wa utaratibu mpya wa upangaji wa miji na kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi chuo kimehuisha miongozo ya upangaji miji hapa nchini

Hili ni eneo lingine muhimu la utafiti ambalo wasomi wanapaswa kuwekeza kwa nguvu kubwa kwani miji mingi hapa nchini imejengwa holela ni maeneo machache sana ambayo yamejengwa kwa mpangilio unaotambuliwa na serikali.

Wananchi wamevamia maeneo mengi kabla ya serikali kupanga hivyo wasomi wanapaswa waje na majibu ya suala hili kwa kutengeneza miongozo itakayosababisha miji mingi hapa nchini ipangiliwe upya kwa kuwekwa miundombinu itakayosababisha maeneo hayo yafikike.

Maeneo ambayo hayajafanywa makazi bado ni mengi nchini hivyo wasomi wakija na mpango mzuri wa namna ya kuyapanga maeneo hayo kabla ya kuvamiwa na wananchi ili yajulikane maeneo ya wazi, barabara na mitaa tofauti na ilivyo kwenye baadhi ya miji ambayo haifikiki kutokana na kutopangiliwa

Hivyo basi kuna umuhimu mkubwa wasomi wetu badala ya kuishia kufundisha kwenye vyuo vya elimu ya juu wakajikita kufanya tafiti mbalimbali waisaidie nchi kufikia malengo yake ya kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa juu kwakuja na tafiti nyingi zitakazotoa majibu ya matatizo yaliyopo.



Mkuu wa Chuo Kikuu Ardhi (ARU), Cleopa Msuya, akimtunuku Shahada ya Uzamivu mmoja wa wahitimu wa chuo hicho kwenye mahafali ya 14 ya chuo hicho yaliyofanyika chuoni hapo hivi karibuni.

# MIKE MUBUVI SONKO

## •Gavana mvaa mikufu aliyejaa vituko
## •Alianza kwa mbwembwe, akaishia vibaya

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE Bunge la Seneti nchini Kenya, limepiga kura kumuondoa madarakani, Mike Mubuvi Sonko, kama gavana wa jiji la Nairobi.

Hatua hiyo imehitimisha miaka mitatu ya utawala wake ambao ulitawaliwa na utata mwingi na mivutano ya kisiasa.

Sonko ambaye alikuwa gavana kijana alituhumiwa kwa makosa mbalimbali ikiwamo ukiukaji wa katiba, matumizi mbaya ya mamlaka, utovu wa nidhamu na ufisadi.

Jumla ya maseneta 27 walipiga kura kuunga mkono kuvuliwa uongozi kwa Sonko, baada ya kukubaliana na mashtaka yote manne yaliyowasilishwa na Bunge la Kaunti ya Nairobi, ambalo lilipiga kura ya kutokuwa na imani naye mnamo Desemba 3 mwaka huu.

Kuondolewa kwa Sonko, imempa nafasi Spika wa Bunge la Kaunti ya Nairobi, Ben Mutura, kukaimu wadhifa huo hadi uchaguzi wa gavana na naibu wake utakapofanyika ndani ya siku 60 zijazo.





**SONKO NI NANI?**

Kiongozi hiyo ni maarufu nchini Kenya na anajulikana kutokana na vituko vyake.

Hivi karibuni maofisa wa magereza nchini humo walimshtaki Soko kutokana na hatua yake ya kutoroka akiwa kifungoni miaka 20 iliyopita.

Hata hivyo, Sonko mwenyewe amekiri hadharani kutoroka jela wakati alipofanya mahojiano ya moja kwa moja na kituo kimoja cha runinga.

**JINA LAKE MAARUFU**

Jina la Soko lina umaarufu hasa kwa vijana ambao wanamuona kama sehemu yao, na mara kadhaa wanajumuika naye katika matukio mbalimbali ya kijamii.

Sonko alijipatia umaarufu kutokana na mtindo wake usio wa kawaida alipokuwa Mbunge wa Makadara, jijini Nairobi.

Anafahamika kwa kuvalia vito vya thamani kama mikufu na bangili za dhahabu.

Katika kituko kimoja, gavana huyo aliwahimiza vijana kutumia pombe kama kitakasa mikono kama njia ya kuvikinga na Covid-19.

Yeye mwenyewe alikusanya chupa za pombe aina ya Hennessy kama sehemu ya kifurushi cha kujitakasa cha kupambana na virusi vya corona na kuwasambazia wakazi wa jiji hilo.

Sonko alidai kiwango cha pombe katika kinywaji hicho kinaweza kuzuia virusi vya corona.

MISUKOSUKO YA KISISASA

Misukosuko ya kisiasa ilifikia kilele mwezi Novemba baada ya kukamatwa akituhumiwa ufisadi.

Sonko alichaguliwa kuwa Gavana wa Kaunti ya Nairobi mwaka 2017, kupitia chama cha Jubilee cha Rais Uhuru Kenyatta.

Hata hivyo, uhusiano wake na Rais Kenyatta, uliingia doa baada ya kutofautiana kuhusu mageuzi yaliyosababisha majukumu mengi ya Kaunti ya Nairobi kuhamishiwa serikali kuu.

Rais Kenyatta, alimteua jenerali wa kijeshi kuendesha shughuli za kaunti, hali iliyomfanya Sonko kuwa gavana asiye na mamlaka.

Katika mabadiliko hayo, Sonko, alishiriki hafla ya kukabidhi mamlaka serikali kuu, lakini baadae alipinga na kudai alisaini nyaraka za makabidhiano akiwa katika hali ya ulevi, hivyo si halali.

**SAFARI YAKE YA KISIASA**

Alipokuwa mbunge, aliandaa maandamano ya kudai haki ya wanyonge na wafanyabiashara ndogondogo ambao walikuwa wakikamatwa na kufukuzwa kutika maeneo muhimu ya jiji hilo.

Atakumbukwa pia kwa kuongoza waandamanaji Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Jinai (ICC) The Hague, Uholanzi akitaka kesi dhidi ya Rais Uhuru Kenyatta, ifutwe na baadae shauri hilo likasitishwa.

Alipokuwa Seneta, alianzisha kundi lake aliloliita Sonko Rescue Team' ambalo lilikuwa na kazi ya kutoa huduma ya maji, matibabu na misaada wakati wa mazishi.

Wakati mmoja alipoitwa kusaidia familia zilizokuwa zimeathiriwa na bomoa bomoa jijini mwaka 2014, alimpigia simu Rais Kenyatta na kumuweka kwenye kipaza sauti na alitoa agizo ubomoaji huo usitishwe.

Alipoingia uongozini alionekana kuchukua hatua ambazo zinaenda kinyume na aliyokuwa akitetea.

**Kwa msaada wa BBC.**



## HABARI KIMATAIFA

# Buyoya afariki dunia uhamishoni

**PARIS,** Ufaransa

RAIS wa zamani wa Burundi, Pierre Buyoya, amefariki dunia akipatiwa matibabu ya Covid-19 nchini Ufaransa.

Kwa mujibu binamu yake na chanzo cha kidiplomasia, Buyoya (71) (pichani) alifariki mjini Paris, siku ya Alhamisi baada ya kukimbizwa hospitali kwa ajili ya matibabu.

Jenerali huyo mstaafu alihudumu nafasi hiyo mara mbili kwa wa jumla ya miaka 13 baada ya kuwapindua madarakani watangulizi wake.

Mwezi Oktoba, mwaka huu, kiongozi huyo alihukumiwa mahakama kuu ya Burundi, kifungo cha maisha gerezani baada ya kupatikana na hatia ya mauaji ya Rais wa kwanza aliyechaguliwa kidemokrasia nchini humo, Melchior Ndadaye mwaka 1993.

**Mwezi uliyopita, alijiuzulu kama mjumbe wa Muungano wa Afrika, anayeshughulikia eneo la Sahel, akieleza anataka kutumia muda wake kusafisha jina lake.**

Mapinduzi hayo yalisababisha vurugu na kupoteza maisha ya watu 300,000.

Hata hivyo, Buyoya alikana makosa hayo akilalamika yanatokana na mambo ya kisiasa.

Mwezi uliyopita, alijiuzulu kama mjumbe wa Muungano wa Afrika, anayeshughulikia eneo la Sahel, akieleza anataka kutumia muda wake kusafisha jina lake.

Marehemu Pierre Buyoya aliingia madarakani kwa mara ya kwanza baada mapinduzi ya kijeshi dhidi ya utawala wa Rais Jean-Baptiste Bagaza mwaka 1987. Utawala wake wa miaka sita uligubikwa na matukio mengi ambayo yalibadili sura ya nchi, kama vile mauaji ya kinyama yaliyofanyika katika kitongoji cha Ntega-Marangara mwaka 1988.



Hata hivyo, makubaliano ya umoja wa kitaifa yalifikiwa mwaka 1991, na mwaka 1993 kuliainishwa mfumo wa vyama vingi.

Mwaka 1993, aliondoka madarakani baada ya kushindwa katika uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi na Melchior Ndadaye alichukua uongozi kutoka chama cha Frodebu.

Buyoya alirejea tena madarakani Julai 1996, baada ya kumpindua tena Rais wa mpito Sylvestre Ntibantunganya, ambaye wakati huo alichukua madaraka kufuatia kifo cha Cyprien Ntaryamira ambaye alikufa katika ajali ya ndege pamoja aliyekuwa Rais wa Rwanda Juvenal Habyarimana.

Hali hiyo ilimlazimu Buyoya kufanya mazungumzo na wapinzani wa serikali waliokuwa wameanzisha vita , mazungumzo yaliyodumu kwa muda wa miaka miwili.

Buyoya alikubaliwa kuhudumu kwa kipindi cha mpito kutekeleza makubaliano ya amani ya Arusha na baadaye akaondoka madarakani mwaka 2003 na uongozi wa nchi ukawa chini ya Domitien Ndayizeye.

Mwaka 2008, aliteuliwa kuwa mjumbe maalum wa amani Umoja wa Mataifa katika nchi ya Mali na Sahel kufuatia mzozo wa kivita kati ya Mali na nchi jirani ya Sudan. **BBC**

# Wanafunzi 344 Nigeria waachiwa huru

**ABUJA,** Nigeria

NIGERIA imetangaza kuachiwa huru kwa wanafunzi wa kiume 344 waliotekwa nyara wiki iliyopita na wanamgambo wa makundi ya itikadi kali ya Kiislam kaskazini magharibi mwa nchi hiyo.

Gavana wa jimbo la Katsina, Aminu Masari (pichani chini), alitoa tangazo hilo jana akisema wanafunzi hao waliachiwa huru na tayari wamekabidhiwa kwa vikosi vya usalama, ambavyo vimewasarifisha hadi makao makuu ya jimbo hilo.

Masari alisema wanafunzi hao watafanyiwa uchunguzi wa kitabibu kabla ya kukabidhiwa kwa familia zao na kuahidi serikali itashirikiana na vikosi vya usalama kuzuia tukio kama hilo kutokea tena.

Zaidi ya wanafunzi 800 walikuwapo katika shule ya sayansi ya serikali kwenye mji wa Kankara wakati wanamgambo walipoivamia na kuwateka zaidi ya wanafunzi 400. **DW**





Mkazi mmoja akionyesha nyumba yake iliyoanguka baada ya kimbuka Yasa kukipiga Kisiwa cha Fiji juzi. **PICHA: AFP**

# Kimbunga Yasa chaipiga Fiji

**SUVA,** FIJI

WATU wawili wamekufa na wengine 23,000 wamejeruhiwa baada ya kimbunga kikali kilichopewa jina la Yasa kukipiga kisiwa cha Fiji.

Kimbunga hicho cha ngazi ya tano kilisababisha uharibifu majengo, mashamba na miundombinu mbalimbali

Kituo cha radio cha nchi hiyo kilimnukuu mkurugenzi wa ofisi ya kudhibiti majanga, Vasiti Soko, akisema vifo vya watu hao wawili vimethibitishwa wakati kimbunga Yasa kilipowasili kisiwani humo kikiwa na kasi ya kilomita 345 kwa saa.

Mbali ya kusababisha mafuriko kwenye maeneo mengine ya kisiwa hicho, kimbunga Yasa, ambacho ni kikali zaidi kuwahi kuipiga Fiji, kimefanya uharibifu mkubwa kwenye mashamba ya mazao.

Hata hivyo, nchi jirani ya New Zealand imeahidi kutuma msaada wa fedha na ushauri wa kiufundi kwa Fiji.

Waziri Mkuu wa kisiwa hicho, Frank Bainimarama, alisema kimbunga Yasa ni dalili ya kuwapo dharura ya kimazingira duniani. **DW**

# China, Marekani zaonyeshana ubabe

**BEIJING,** China

SERIKALI ya China imesema inapinga vikali mwenendo wa Marekani wa kuituhumu nchi hiyo bila ya kuwa na ushahidi na kuzilenga kampuni zake.

Kauli hiyo imetolewa na msemaji wa Wizara ya Mambo ya Kigeni wa China, Wang Wenbin, wakati akijibu hatua ya Marekani ya kuzipiga marufuku kampuni zinazosambaza umeme kwenye miundombinu ya ulinzi ya Marekani kununua vifaa pamoja na vipuri kutoka China.

Juzi Waziri wa Nishati wa Marekani alitia saini amri ya kuzuia kampuni hizo kuagiza aina kadhaa ya vifaa kutoka China kama sehemu ya juhudi ya kulinda usalama wa Marekani dhidi ya udukuzi na mashambulizi mengine ya kimtandao.

Uamuzi huo umeikasirisha serikali ya China, ambayo ilisema nchi hiyo itaendelea kuchukua hatua zinazohitajika kulinda haki na maslahi ya kampuni zake. **DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam - 0768 928 516.**
**Arusha - 0677 226 960.**

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

## TUNAHITAJI MAFUNDI

**TUNAHITAJI MAFUNDI WA PIKIPIKI WENYE UZOEFU, UMRI MIAKA 25-35.**
**TUMA MAOMBI KWA: linkallafrica@gmail.com**
**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI: 17/12/2020.**

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PAMOJA MINING CO. LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T470 DEE** AINA YA TOYOTA HILUX. YENYE ENGINE No. **1KD7553650 CHASSIS AHTF229G609024801.** KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI: **KAH/TR/RB/444/2020.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5**
**KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;375/2020**
Ombi la **ABDUL R.SIARA**,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **FATUMA SAID ABDALLAH.**Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo **tarehe 22/12/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa **tarehe 10/12/2020.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5**
**KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;351/2020**
Ombi la **EDWARD KENEDY,**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **KENEDY PETRO AUGUSTINO.**Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo **tarehe 18/12/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa **tarehe 18/11/2020.**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**SHAURI LA MAOMBI NAMBA 84 YA MWAKA 2020**
**(SHAURI ASILIA MADAI NO 46/2019**

**PUNUNTA'S COMPANY LIMITED............MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**EMMANUEL MANONI.....................MJIBU MAOMBI**

**KWA: MDAIWA**
**POPOTE ULIPO**
Mahakama hii inakufahamisha kwamba Mdai amefungua shauri la Maombi ya kukaza Hukumu dhidi yako, nakala yake inapatikana katika Mahakama hii.
Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo **tarehe 13/01/2021 saa 2:30** asubuhi na unatakiwa kuwepo, au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya madai haya.
Zingatia kwamba kutofika kwako tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe kutaarifiwa tena, na maamuzi kutolewa,
Imetolewa kwa mkono wangu na Mhuri wa mahakama hii leo **tarehe 10/12/2020.**
**HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI MFAWIDHI**
**MWANZA**

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB:
+255 - 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

## Mauaji Harusini-**43**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

"Abesh Abdallah." Alijibu Tamim na kujiona ametua mzigo mzito uliokuwa unamuelemea.

Eddy aliduwaa. Hakutegemea kama Tamim atalitaja jina hilo.

Ni jina la mtu mzito. Mfanyabiashara mkubwa nchini anayefahamika hata na watoto wadogo.

Ni mfanyabiashha ambaye umaarufu wake mkubwa ni mabasi ya kusafiri mikoani.

Hii ilimfanya kwa mbali Eddy atetemeke. Sababu iliyotajwa ya kimapenzi, ilimfanya Eddy kujua kuwa kumbe shangazi yake kabla ya kufunga ndoa ya Patiyo alikuwa ni mpenzi wa Abesh.

Kumbe ilikuwa ni kesi ya matajiri wawili waliochukuliana wapenzi.

Wakati Tamim alieleza, Eddy alikuwa akirekodi kwenye simu yake maalum ya mkononi kwa ajili ya ushahidi.

Tayari kitu kilichopo mkononi mwake ni kuwa wauaji wa Patiyo na Grace na waliotaka kumuua Shani ni hao hao. Ila Jim, George, Ben na Paul siyo wao waliotaka kumuua ndugu yao kwa ajili ya mali.

Grace na Patiyo waliuawa kwa ugomvi wa kimapenzi, lakini wao walitaka kumuua Shani kwa sababu ya kutaka kurithi mali ya kaka yao kwa sababu tu alikuwa na binti huyo tu pekee.

Mlango ulifunguka. Amour aliingia na wenzake watatu. walikuwa wameongozana na watu wengine wawili ambao Eddy hakuwafahamu.

"Bosi hawa wawili ni Jim na Ben ambao walikuwa wametoroka. Tumewakamata leo. Hawa wanatakiwa kuunganishwa kwenye kesi ya George na Paul ya kutaka kumuua Shani." Amour alimhabarisha.

"Na huyu na wenzake, watanatakiwa kufunguliwa kesi mbili. Moja ya kujaribu kuua. na nyingine ni kuwaua watu wawili, Patiyo na Grace. Lakini leo hii mnatakiwa mkamkamate mtu mmoja anaitwa Abesh Abdallah, sawa?"

****************************

"Kwa nini mpenzi hukuniambia?" Ilikuwa ni sauti ya kwikwi kutoka kwa Shani.

"Nisingeweza kukwambia kabisa?"

"Kwa nini, kwa nini Sherry?"

"Kwanza kabisa sikutaka uwe na hofu. Ungejua kama baba zako wadogo wanataka kukuua kwa sababu warithi mali za marehemu baba yako, kwanza huenda usingeniamini japo, uliwahi kuniambia kuwa huishi nao kwa amani sana. Halafu Sherry sikutaka kukufanya uishi kwa mashaka. Hebu fikiria sakata hili lipo mwaka mzima sasa, ungeishije wewe?"




**Abesh, Jim na kundi lao wamekamatwa, nadhani yamekwisha sasa. Kilichobaki nakuahidi pamoja na kazi niliyonayo, lakini sasa nakubali kuchukua jukumu la kuendesha biashara na mali zote za baba yako. Lakini sitafanya hivyo hadi nikuoe.**

"Kumbe hata siku ile uliponikataza nisile kile chakula, ukaagiza kingine na kuniambia tutakile tukimaliza kile uliochoagiza mara ya pili, tayari ulikuwa umegundua mpango wa kunidhiru kwa sumu?" Shani alikuwa akiuliza maswali akiwa amemkumbatia kwa nguvu Eddy.

"Ndiyo, ilikuwa hivyo, Fikiri ambaye alikuwa anakuhudumia ndiye aliyepewa pesa na baba zako wadogo, George, Jim, Ben na Paul ili akuwekee sumu ufe, warithi mali za baba yako, na baadaye walimpa pesa mhuni mmoja anaitwa Timo, akamuua Fikiri ili asije kutoa siri, lakini pia wasimmalizie pesa, wakidhani kuwa tayari wameshakupa sumu."

Shani aliendelea kububujikwa na machozi. Aliona kama anaota ndoto. Tena ndoto ya mchana kweupe.

Siku zote alikuwa akiishi na mwanaume. Mwanaume aliyetokea kumpenda mno tangu amuone kwa mara ya kwanza Kinondoni makaburini alipokwenda kusali kwenye kaburi la baba yake Patiyo.

Alimuona kijana mmoja mtanashati ambaye naye alikuwa anasali kwenye kaburi la Grace. Grace huyo huyo ndiye mke wa baba yake ambaye waliuawa wote wakati wanatoka kufunga ndoa.

Walisalimiana na kufahamishana. Ndipo Shani alipogundua kuwa kijana yule alikuja kwenye kaburi la shangazi yake ambaye wakati anauawa yeye alikuwa masomoni nchini Marekani.

Maneno aliyoongea makaburini hapo yalimfanya aondokee kumhusudu kijana yule na kuamua kujiweka karibu naye.

*********************

"Wewe mwenyewe unaitwa nani?"

"Naitwa Shani."

"Baba yako alikuwa anaitwa nani?"

"Patiyo."

"Nadhani ndiyo alikuwa mume wa shangazi yangu."

Shani aliitikia kwa kichwa.

"Pole Shani, najua jinsi unavyoumia kwa kumkosa baba yako kutokana na baadhi ya watu wenye roho mbaya.

Nakuahidi, watu wote waliofanya mauaji haya, na yoyote aliye nyuma ya mpango huu, ni lazima watapatikana na kulipa maovu yote haya." Eddy aliongea kwa sauti ya chini, lakini kwenye mamlaka na msisitizo, ikipenya vema kwenye masikio ya mwanadada Shani.

"Kwani wewe unaitwa nani?" Shani kwa mara ya kwanza naye alimuuliza.

"Naitwa Eddy Kamal"

"Ni askari wewe kwani."

"Hapana, mimi nilikwambia mwanzo nimetoka kusoma Marekani. Kwa sasa sina kazi yoyote ile."

"Uko nyumbani tu?"

"Ndiyo maana yake."

Kwa kipindi kifupi tu, Shani alitokea kumuamini na kupenda staili za kijana huyu mwenye tabia ya kujimini tangu siku hiyo.

Tukio hilo lote liliingia kwenye kichwa cha Shani na kuona kama ilikuwa jana.

"Kumbe maneno yale yote, kumbe ni mpelelezi wa kimataifa?" Alijiambia mwenyewe.

"Mpenzi, kuna vitu vingi ulinificha. Hata kazi yako ulinificha. Uliniambia kuwa wewe ni 'mesheni tauni'. Nilitaka kukupa kazi ya kuendesha biashara zote za baba yangu, ukaniambia nisubiri kwanza, kumbe ni mpelelezi, siamini. Siamini kuwa nilikuwa naishi na mtu maarufu na muhimu nchini Tanzania, siamini." Bado Shani aliendelea kushangaa kwa jinsi mchezo mzima ulivyochezeka.

Kwa akili yake ya kawaida aliamini kuwa mpenzi wake Eddy hakuwa mpelelezi wa kawaida. Tangu alipomuokoa kifo cha sumu kutoka kwa Fikiri bila yeye kujua, hadi alipomtaka kuhama Mbezi Beach na kuhamia Kijitonyama, kumbe ilikuwa ni kwa ajili ya usalama tu, lakini hakumwambia chochote. Alikuwa akimlinda bila kumwambia kitu. Alishajua kuwa baba zake wadogo wanamuwinda wamuue, lakini pia hakumwambia. Hata siku ambayo walikuwa wakifukuzwa na magari na bodaboda kwa ajili ya kuuawa. aliyekuwa ajua mchezo mzima wa nini kiaendelea ni Eddy tu. Hata siku alipovamia nyumbani kwake Mbezi Beach na watu ambao walidhaniwa kuwa ni majambazi, kumbe Eddy alijua nia ya wale watu na walitumwa na nani, lakini alimficha.

"Nisingeweza kukwambia kuwa mimi ni mpelelezi mpenzi. Umejua sasa kwa sababu tayari mambo yameisha. Kujua kwako mapema kungeweza kabisa kuifanya kazi hii kuwa ngumu zaidi kwangu na isingefika hapa ambapo wahalifu wote wamekamatwa na kesho wanapelekwa mahakamani." Eddy alimwambia mpenzi wake.

Shani alijua yote haya, baada ya kusikia kila kitu kwenye taarifa ya habari ya ITV ya saa mbili usiku, juu ya kukamatwa kwa waliohusika kumuua Patiyo na mkewe Grace mwaka mmoja uliopita na sababu ya kufanya hivyo, lakini pia waliotaka kumuua binti ya Patiyo Shani. Waliomuua Patiyo na mkewe ni sababu ya mapenzi na waliotaka kumuua binti yake ambao ni baba zake wadogo ni sababu ya mali.

"Abesh, Jim na kundi lao wamekamatwa, nadhani yamekwisha sasa. Kilichobaki nakuahidi pamoja na kazi niliyonayo, lakini sasa nakubali kuchukua jukumu la kuendesha biashara na mali zote za baba yako. Lakini sitafanya hivyo hadi nikuoe."

"Utanioa Eddy?"

"Hilo ni jibu Shani, pigia msitari, nakupenda sana."

Machozi yalimtiririka Shani na mwili ukakosa nguvu kwa furaha.

Eddy, nikiongea kingine chochote itaonekana kama nakosea. Nachoweza kusema kimoja tu. Nami pia nakupenda sana.

**MWISHO**

# MAN UTD YAIFUATA CHELSEA KWA RICE




**LONDON,** England

KLABU ya Manchester United imeripotiwa ipo tayari kuipa changamoto Chelsea katika kumwania kiungo wa West Ham, Declan Rice.

Rice mwenye umri wa miaka 21, amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kwenda Stamford Bridge, lakini halikuweza kuzaa matunda. United ipo tayari kuingia kwenye mbio za kumwania nyota huo wa kimataifa wa England.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Express, Man United ipo tayari kumsajili nyota huyo ambaye Chelsea wamekuwa wakimuwania kwa muda mrefu.

Ripoti zinaeleza kuwa, kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer ni shabiki mkubwa wa Rice, ambaye wakati wa utoto wake alicheza katika akademi ya Chelsea.

# Klopp kocha bora wa FIFA

**ZURICH,** Uswisi

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, ametajwa kuwa kocha bora wa 2020 katika tuzo ambazo zimetolewa na FIFA Alhamis ya Desemba 17 akimtupa mbali kocha wa Bayern Munich, Hansi Flick.

Klopp baada ya kutajwa kama kocha bora, amesema hakutegemea kama angeitwa na kutajwa kama kocha bora "ilinishitua".

Juhudi kubwa kwa kocha Klopp ni pamoja na kukiongoza kikosi cha 'Majogoo' wa Merseyside, Liverpool kushinda taji la Ligi Kuu nchini humo kwa mara ya kwanza baada ya takribani miaka 30 ya ukame wa taji la EPL.

Inakuwa mara ya pili mfululizo kwa Klopp kutajwa kuwa kocha bora wa mwaka wa FIFA.

Mjerumani huyo alishinda tuzo kama hiyo mwaka 2019 baada ya kubeba Kombe la Mabingwa Ulaya kwa kuifunga Tottenham na kwa awamu hii Klopp amempiku mpinzani wake wa karibu ambaye ni kocha wa Bayern Munich, Hans Flick na Marcelo Bielsa wa Leeds United.

"Nilishitushwa kusikia jina langu" alisema. "Nina watu wengi wa kuwashukuru na makocha wangu".





# *Lewandowski mchezaji bora wa dunia*

**ZURICH,** Uswisi

ROBERT Lewandowski ameshinda tuzo kubwa kabisa ya taaluma yake, na kudhihirisha kuwa mshambuliaji ambaye si Lionel Messi au Cristiano Ronaldo anaweza kupigiwa kura ya kuwa mchezaji bora wa kandanda duniani.

Nahodha huyo wa Poland ameshinda tuzo ya Mchezaji Bora wa FIFA kwa Mwanaume katika mwaka wa 2020 baada ya mabao yake 55 ya msimu kuisaidia Bayern Munich kunyakua mataji matatu msimu uliopita.

Lewandowski alipata kura 52 dhidi ya 38 alizopata Messi wakati Ronaldo akipata 35.

Hafla ya tuzo hiyo ilifanyika Zurich kwa njia ya video, lakini Rais wa FIFA, Gianni Infantino, alikwenda hadi Munich kumkabidhi binafsi Lewandowski tuzo yake.

Lucy Bronze wa Uingereza alishinda tuzo hiyo kwa upande wa wanawake.

Bronze alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Lyon kabla ya kuhamia Manchester City.

HABARI MICHEZO

# Mourinho: Liverpool wanabebwa EPL

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Tottenham, Jose Mourinho, amesema ushindi ambao wameupata wapinzani wao, Liverpool kwenye mchezo wa Ligi Kuu England ni wa kutengenezwa jambo ambalo halimpi tabu.

Ikiwa Uwanja wa Anfield ilikubali kichapo cha mabao 2-1 mbele ya Liverpool na kuifanya Tottenham kupoteza mchezo wa pili ndani ya Ligi Kuu England.

Roberto Firmino kichwa chake cha dakika ya 89 kilipeleka msiba mazima ndani ya Tottenham na lile bao la kwanza kwenye mchezo huo lilipachikwa na nyota Mohamed Salah dakika ya 26 huku la kufutia machozi kwa Tottenham likifungwa na Son Heung-min dakika ya 33.

Ushindi huo unaifanya Liverpool ya Klopp kuwa nafasi ya kwanza ikiwa na pointi 28 huku Tottenham ikiwa nafasi ya pili na pointi zake 25.

Mourinho amesema: "Ushindi walioupata ni kutokana na makosa ambayo tumeyafanya kwenye kumalizia nafasi kwa sababu tulipata nafasi nyingi tukashindwa kuzitumia.

"Hakuna namna ni ushindi wa kutengenezwa ndani ya uwanja, wao walikuwa na presha kubwa na walikuwa wanahitaji kuongoza ligi wamefanikiwa.

"Nimemwambia Klopp kwamba ameshinda mbele ya timu kubwa ambayo ilistahili kushinda ndani ya Anfield, siwezi kubadili matokeo kwa sasa kwa kuwa yameshatokea."






# SOLSKJAER 'AWAJAZA UPEPO' WACHEZAJI

**MANCHESTER,** England

BAADA ya ushindi wa mabao 3-2, walioupata Manchester United mbele ya Sheffield United wakiwa ugenini, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ole Gunner Solskjaer, amesema mabao yote matatu yalikuwa bora na yenye viwango.

David Mcgoldrick wa Sheffield United alianza kupachika bao mapema dakika ya tano na alipachika la pili dakika ya 87 huku yale ya United yakipachikwa nyavuni na Marcus Rashford aliyefunga mawili dakika ya 26 na 51 na moja lilifungwa na Anthony Martial dakika ya 33.

Wakiwa ndani ya Uwanja wa Bramall Lane, United ilisepa na pointi tatu na kuifanya ifikishe jumla ya pointi 23 ikiwa nafasi ya 6 baada ya kucheza mechi 12 huku Sheffield United ikiwa nafasi ya 20 na pointi moja baada ya kupata sare moja ikiwa imecheza jumla ya mechi 13.

Imeachwa kwa pointi tano na vinara wa Ligi Kuu England ambao ni mabingwa watetezi, Liverpool wakiwa na pointi 28 baada ya kucheza mechi 13.

Ole amesema: "Uwezo mkubwa, kila mmoja amepambana na kufanya vizuri, mabao yote ni bora na yenye viwango."

# *Messi, Ronaldo waunda kikosi bora cha FIFA*


**ZURICH,** Uswisi

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa (FIFA), limetoa tuzo zake katika kutambua thamani ya kila mchezaji na kuongeza ushindani.

FIFA ilitangaza pia kikosi cha msimu katika mashindano yote.

Katika kikosi ambacho kimetangazwa mjini Zurich, Uswisi, mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo na yule wa FC Barcelona Lionel Messi, wamefanikiwa kuingia ikiwa ni mara nyingi zaidi tangia mwaka 2007.

Mlinda mlango wa Liverpool, Allison Becker, licha ya kukosa nafasi ya kutwaa tuzo ya kipa bora bado ametajwa kwenye kikosi hicho, majina ya kikosi haya hapa; Alisson (Liverpool), Trent Alexander-Arnold (Liverpool), Virgil van Dijk (Liverpool), Sergio Ramos (Real Madrid), Alphonso Davies (Bayern Munich), Joshua Kimmich (Bayern Munich), Kevin de Bruyne (Manchester City) Thiago (Liverpool), Lionel Messi (Barcelona), Robert Lewandowski (Bayern Munich) na Cristiano Ronaldo (Juventus).



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO AMCHAGUA MESSI, LEWANDOWSKI ABEBA TUZO

## Ni ya mchezaji bora wa FIFA, nyota huyo wa Barca yeye amtosa, lakini...

**ZURICH,** Uswisi

CRISTIANO Ronaldo amewashangaza wengi kwa kumchagua mpinzani wake mkubwa Lionel Mess wa Barcelona katika orodha ya wachezaji watatu bora wa kuwania tuzo ya Mhezaji Bora wa mwaka wa FIFA.

**Katika orodha hiyo, Ronaldo alimuweka nyota wa Bayern Munich, Robert Lewandowski kuwa namba moja, huku Messi akimuweka nafasi ya pili.**

Lewandowski straika wa kimataifa wa Poland alishinda tuzo hiyo baada ya kuwa na msimu mzuri na miamba wa 'Bavaria' kwa msimu uliopita.

Lewandowski aliiongoza Bayern Munich kushinda mataji matatu msimu uliopita pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Huku tuzo za Ballon d'Or 2020 zikiwa zimefutwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, tuzo ya FIFA ndio ilibaki kuwa tuzo kubwa kwa mchezaji binafsi.

Wakati Lionel Messi alishinda tuzo hiyo mwaka 2019, Cristiano Ronaldo ameshinda mara mbili (2016 na 2017).

Luka Modric ndiye mchezaji pekee kuibeba tuzo hiyo nje ya Messi na Ronaldo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016.

Baada ya sherehe ya tuzo hizo kwenye makao makuu ya za FIFA mjini Zurich, yalitolewa maelezo namna wachezaji walivyochaguana.

Ronaldo alimuweka Lewandowski namba moja, huku Messi na Kylian Mbappe akiwaweka nafasi ya pili na tatu. Nyota huyo wa Juventus aliweka upinzani wake na Messi pembeni na kuamua kumchagua nahodha huyo wa Barcelona.

Hata hivyo, kwa upande wa Messi mchezaji wa kimataifa wa Argentina hakumuweka Ronaldo kwenye orodha yake ya wachezaji watatu, kwani alimchagua Neymar Jr na Kylian Mbappe huku namba moja akimuweka Lewandowski.

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTAKA RICE

KLABU ya Manchester United huenda wakawasilisha dau la kumnunua kiungo wa kati wa West Ham, Declan Rice mwenye umri wa miaka 21, japo mchezaji huyo anadhaniwa kutaka kujiunga na Chelsea endapo ataamua kuondoka kwa wagonga nyundo hao wa London. ***(Express)***

### ORIGI KUONDOKA LIVERPOOL

WOLVES inamfuatilia mshambuliaji wa Liverpool na Ubelgiji, Divock Origi mwenye umri wa miaka 25, ambaye huenda akaruhusiwa kuondoka Januari. ***(Mail)***

### ROJO KUONDOKA UNITED

MANCHESTER United wanashughulikia mchakato wa Marcos Rojo kuondoka klabuni hapo Januari, huku Newcastle wakipania kumsajili kwa mkopo mlinzi huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 30. ***(The Athletic)***

### IBANEZ AWANIWA LIVER

LIVERPOOL wamemuongeza mchezaji wa AS Roma kwenye safu ya ulinzi, Roger Ibanez, katika orodha ya walinzi wanaosakwa kujaza pengo lililoachwa na mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi, Virgil van Dijk mwenye umri wa miaka 29, ambaye ni majeruhi na huenda wakawasilisha dau la pauni milioni 30 kumnunua Mbrazili huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(AS Roma Live, via Team Talk)***

### FONT KUTORUDIA MAKOSA

MGOMBEA Urais wa Barcelona, Victor Font, amesema hatarudia makosa yaliyofanywa na watangulizi wake kutangaza nia ya kuwanunua wachezaji nyota licha ya kuhusishwa na tetesi za kumnyatia mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 20. Lakini anapanga kumshawishi Lionel Messi mwenye miaka 33, kusaini mkataba mpya. ***(Goal)***

### SZOBOSZLAI AITOSA ARSENAL

KIUNGO wa Hungary, Dominik Szoboszlai mwenye miaka 20, anayenyatiwa na Arsenal, amekamilisha uhamisho wa kutua RB Leipzig kutoka klabu dada ya Red Bull Salzburg, na anatarajiwa kujiunga nayo Januari baada ya kusaini mkataba wa mika minne na nusu. ***(Mirror)***

### ANCELOTTI SASA NA MATAJI

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, ana matumaini ya kukamilisha mkataba wake katika klabu hiyo kwa "ushindi wa mataji" katika kipindi cha muda atakaokuwa hapo hadi mwishoni mwa msimu wa 2023-24. ***(Liverpool Echo)***

### NAPOLI YAMTAKA MILIK

KLABU ya Napoli itaitisha angalau pauni milioni 14 kumuuza mshambuliaji wa Poland, Arkadiusz Milik, katika dirisha la Januari licha ya mchezaji huyo kunyatiwa na Juventus na Atletico Madrid. Milik mwenye umri wa miaka 26-pia ananyatiwa na Everton. ***(Goal)***

### ARSENA YAMNAYIA REKIK

KLABU ya Arsenal inaonekana inakaribia kukamilisha usajili wa mchezaji wa Hertha Berlin, Omar Rekik baada ya mlinzi huyo aliye na umri wa miaka 18 kuwasili mjini London juzi, Alhamisi. ***(Metro)***

HABARI MICHEZO

# Fifa yawapa beji waamuzi 17 Tz

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa (FIFA), limetoa beji kwa waamuzi 17 wa Tanzania kwa mwaka 2021.

Kwa mujibu wa orodha ya Fifa iliyotumwa Shirikisho la Soka nchini (TFF), inaonyesha waamuzi wa kati sita, waamuzi wasaidizi tisa na wawili wa soka la ufukweni (beach soccer), ndiyo waliopata beji hiyo ya Fifa.

"Waamuzi wa kati ni Florentina Zablon, Hery Sasii, Jonesia Rukyaa, Martin Saanya, Mfaume Nassoro na Ramadhani Kayoko," ilieleza taarifa hiyo.

Na kwa upande wa waamuzi wasaidi iliwataja kuwa ni Abdulaziz Ally, Ferdinand Chacha, Frank Kombe, Hellen Mduma, Janet Balama, Kassim Mpanga, Mbraka Haule, Mohamed Mkono na Soud Lila.

Katika soka la ufukweni, waamuzi waliopewa beji hiyo ya Fifa ni Geofrey Tumaini na jackson Msilimbo.

# Hitimana ataja pakuanzia Mtibwa

**Na Saada Akida**

KOCHA mpya wa Mtibwa Sugar, Thiery Hitimana, amesema aliifuatilia timu hiyo wakati ikicheza baadhi ya mechi zake na kuona tatizo lililokuwa likiisababishia kushindwa kupata matokeo katika mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hitimana ambaye ameridhi mikoba ya Zuberi Katwila, aliyejitimkia Ihefu FC, alisema matatizo aliyoyaona ni katika safu ya ushambuliaji, kiungo na beki wa kati, na kuahidi kuyafanyia kazi kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo lililofunguliwa Desemba 16, kabla ya kufungwa Januari 15, mwakani.

Akizungumza na gazeti hili kwa simu kutoka Morogoro jana, Hitimana alisema baada ya kumalizana na viongozi wa Mtibwa Sugar, amewapa mapendekezo hayo ya usajili kuimarisha kikosi cha timu hiyo.

"Nimeanza kazi rasmi, Mtibwa baada ya kumalizana na kusaini mkataba wa mwaka mmoja na nimependekeza usajili wa nafasi tatu ikiwamo safu ya ushambuliaji". "Nimefuatilia mechi zote za Mtibwa Sugar, wanacheza vizuri, shida wanashindwa kumalizia nafasi wanazotengeneza uwanjani ," alisema Hitimana ambaye mchezo wake wa kwanza kuiongoza timu hiyo utakuwa leo dhidi ya JKT Tanzania.

# MAHADHI, DIDA WATUA IHEFU, ILAMFYA, MIRAJI NAO WATAJWA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Ihefu imezidi kujidhatiti kwa kuimarisha kikosi chake kipindi hiki cha dirisha dogo, baada ya kuwasajili wachezaji Juma Mahadhi kutoka Yanga na golikipa Deogratius Munishi 'Dida' ambaye ni mchezaji huru.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Ihefu, Zagalo Chalamika, amesema wamekuwa na orodha ya wachezaji kadhaa ambao wanataka kuwasajili, lakini kwa kuanzia tayari wamewasajili wachezaji watatu, Dida, Mahadhi na Joseph Mahundi kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao ambacho hakikuwa kwenye wakati mzuri sana katika mechi nyingi za mzunguko wa kwanza.

"Mahadhi tumemchukua kwa mkopo kutoka Yanga, Dida tumemsajili kwa sababu kocha wetu Zuberi Katwila ametuambia kuwa alihitaji kipa mmoja mzoefu, tumemsajili na Mahundi pia," alisema Mtendaji huyo.

Mbali na wachezaji hao, amesema wameiandikia barua klabu ya Simba kuomba wachezaji wawili ambao ni Miraji Athumani na Martin Ilamfya wawachukue kwa mkopo, lakini bado hawajajibiwa.

**"Tumewaandikia barua Simba, hawajatujibu, lakini nadhani watatujibu tu, kama tukiwapata basi itakuwa vizuri sana," alisema.**

Chalamila alisema kuwa lengo ni kufanya vema hasa mzunguko wa pili ili kusalia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Unajua tuliingia kwenye ligi tukiwa wageni, lakini sasa kuna vitu tumejifunza na bado tuna kiu ya kusalia kwenye Ligi Kuu, wamiliki wa klabu bado wanapambana kuhakikisha timu inakuwa bora na kupata wachezaji wazuri watakaokwenda kuongeza nguvu kwenye kikosi kilichopo.

Wakati Ihefu wakisema hayo, Ofisa Habari wa Klabu ya Yanga, Hassan Bumbuli, amekiri kuwatoa wachezaji wawili kwa mkopo, ingawa hakusema wamewapeleka kwenye timu gani.

Tumewatoa wachezaji wetu wawili kwa mkopo, Abdulaziz Makame na Juma Mahadhi, pia mchezaji wetu wa kikosi cha pili Adam Kiondo. Ila kama Kiondo hakupata timu basi tutamrudisha kwenye kikosi cha pili, lakini kila kitu kinaenda kama kilivyopangwa," alisema Bumbuli.

Ihefu ipo katika hali isiyoridhisha Ligi Kuu Tanzania Bara kwani mpaka sasa inashika nafasi ya 17, ikiwa na pointi 10 sawa na Mwadui FC inayoburuza mkia.



Wachezaji wa Namungo FC, wakiwa kwenye boti juzi kuelekea Zanzibar, kuweka kambi kwa ajili ya kujiwinda mechi ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Hilal Obayed ya Sudan, itakayopigwa Jumatano ijayo katika Uwanja wa Azam Comlex, Chamazi jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkutano Mkuu TFF kufanyika Kigoma leo

**Na Somoe Ng'itu,** KIGOMA

MKUTANO Mkuu wa mwaka wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), unatarajiwa kufanyika leo kwenye Ukumbi wa NSSF ulioko Kigoma Mjini, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema maandalizi ya mkutano huo yamekamilika na wajumbe kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na vyama shiriki wanatarajiwa kushiriki.

Kidao alisema katika mkutano huo watajadili taarifa mbalimbali za Utendaji za mwaka uliopita na mipango ya mwaka ujao wa shirikisho hilo linalosimamia soka hapa nchini.

Alisema anaamini wajumbe watakaoshiriki watafanikisha malengo yaliyopangwa na shirikisho hilo kwa ajili ya maslahi ya mpira wa miguu nchini.

"Maandalizi yamekamilika na shirikisho liko tayari kwa mkutano huu wa mwaka wa kawaida, ni mkutano unaofanyika kwa mujibu wa Katiba ya TFF," alisema Kidao.

Aliongeza kabla ya mkutano huo kufanyika, jana kilitangulia kikao cha Kamati ya Utendaji ambacho pia kililenga kupitisha uamuzi na mipango mbalimbali ya shirikisho hilo.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Soka cha Mkoa wa Kigoma (KRFA), Omary Gindi, aliwakaribisha wajumbe wote na kuishukuru TFF kwa kuuchagua mkoa wake kuandaa mkutano huo.

"Binafsi tunaishukuru TFF, Kamati ya Utendaji na Rais Wallace Karia kwa kuleta mkutano Kigoma, unawakaribisha wajumbe wote, ni heshima kubwa tumepata kuwa wenyeji wa mkutano huu, ni mwendelezo wa kupeleka shughuli za soka katika mikoa yote nchini, kama msimu uliopita walivyopeleka fainali za FA Sumbawanga Mjini," Gindi alisema.

Alisema uamuzi wa kupeleka shughuli za soka mikoani ni kutekeleza uamuzi ya kusambaza mpira wa miguu mikoa yote ya Tanzania.

Michezo
Jumamosi Desemba 19, 2020
Nipashe



Ronaldo amchagua Messi, Lewandowski abeba tuzo UKURASA 22

TUMEWAFIKIA...



Wachezaji wa Simba wakiwasili Zimbabwe tayari kwa mechi yao ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji wao, FC Platimum, inayotarajiwa kupigwa Jumatano ijayo nchini humo. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA: PLATINUM HAWANA FIGISU

## ●●● Wafurahia utulivu Zimbabwe ikitua na majembe 24, yasema si kama Nigeria, Sven atoa neno zito...

**Na Saada Akida**

HUKU ikitua Zimbabwe salama na kukuta hali si shwari ya utulivu bila figisufigisu kama ilivyokuwa nchini Nigeria, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amesema anachokitaka ni kumaliza mchezo huo mapema ili kupunguza presha kwenye mechi ya marudiano jijini Dar es Salaam.

**Simba iliondoka na kikosi cha wachezaji 24 jana asubuhi ambacho kilitua salama mjini Harare, Zimbabwe tayari kwa mechi yao ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji, FC Platinum itakayopigwa Jumatano ijayo kabla ya timu hizo kurudiana Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam kati ya Januari 5-6, mwakani.**

Akizungumza na gazeti hili, Sven alisema akili na nguvu zao wanazielekeza katika mchezo huo na tayari kila mchezaji amempa majukumu ya kutafuta matokeo chanya katika mechi hiyo ambayo anaamini itakuwa ngumu kwa kila upande.

Alisema wana kazi kubwa ya kupambana kutafuta matokeo mazuri ugenini na kulingana na majukumu aliyowapa wachezaji wake anaamini utakuwa mchezo mgumu kwa kila upande.

"Kila mchezaji anajua majukumu yake, tunatafuta ushindi katika mchezo huo, tunatambua utakuwa mchezo mkubwa na ushindani kwa sababu wenzetu wapo nyumbani na sisi ugenini.

"Nina kazi ya kufikiria nitakavyoweza kupata matokeo kwenye mchezo dhidi ya FC Platinum, nadhani upo wazi, tuna kazi kubwa kimataifa, tunapambana kupata matokeo mazuri katika mechi iwe ugenini ama nyumbani," alisema Sven.

Alisema kulingana majukumu yaliyopo mbele yao ikiwamo Ligi Kuu, inamfanya asiwe na chaguo hasa kwenye aina ya wachezaji ambao anapaswa kuwatumia.

"Kila mchezaji anatakiwa kuonyesha utulivu na anahitajika kutumika iwe ligi ama michuano ya kimataifa, kufuata maelekezo na majukumu niliyowapa katika mazoezi," alisema Sven.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba (CEO), Barbara Gonzalez, alisema kwa upande wa uongozi wameweka mambo sawa na walitanguliza mtu ikiwa ni pamoja na yeye kuwahi kufika Zimbabwe juzi alfajiri kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya kufikia timu.

Alisema kwa kushirikiana na Balozi wa Tanzania nchini Zimbabwe wameonyeshwa sehemu nzuri na tulivu kwa ajili ya timu hiyo itakapofikia na kufanyia mazoezi kabla ya siku ya mechi.

"Huku hakuna vurugu kama tulizofanyiwa Nigeria, kumepoa hadi sasa hatujaona zile fujo au figisufigisu kutoka kwa wenyeji wetu, tuna imani utakuwa mchezo mzuri na ushindani mkubwa," alisema Barbara.

Wachezaji waliosafiri kwa ajili ya mechi hiyo ni makipa Aishi Manula, Ally Salm na Beno Kakolanya; Mabeki ni Shomari Kapombe, Gadiel Michael, Mohamed Hussein 'Tshabalala', Erasto Nyoni, Ibrahim Ame, Joash Onyango na Pascal Wawa.

Kwa upande wa viungo ni Jonas Mkude, Mzamiru Yassin, Said Ndemla, Taddeo Lwanga, Rally Bwalya, Hassan Dilunga, Francis Kahata na Clatous Chama, huku washambuliaji wakiwa ni John Bocco, Meddie Kagere, Chris Mugalu, Miraji Athumani, Luis Miquissone na Ibrahim Ajibu.

# Ntibazonkiza na mbeleko Yanga kwa Dodoma Jiji

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI akitarajia kumwanzisha kiungo mshambuliaji Saidi Ntibazonkiza katika kikosi cha kwanza leo dhidi ya Dodoma Jiji, Kocha Mkuu wa Yanga, Mrundi Cedric Kaze, amesema anaamini uwapo wake utaongeza kasi na kwa kushirikiana na wenzake ataisaidia timu hiyo kupata matokeo chanya.

Yanga yenye pointi 37 kileleni, zilizotokana na mechi 15, itashuka katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha leo majira saa 10 jioni kuwavaa wenyeji wao Dodoma Jiji wenye alama 19 katika nafasi ya tisa ya msimamo wa ligi hiyo, lakini ikiwa nyuma kwa mchezo mmoja.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu kutoka jijini Arusha jana, Kaze alisema anaupa umuhimu mkubwa mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa mgumu kwa kila upande.

"Nashukuru wachezaji wangu wanaendelea vizuri kujiandaa kukutana na Dodoma Jiji katika mchezo huu ambao hautakuwa rahisi kwa kila upande," alisema Kaze.

Alisema katika mchezo huo mshambuliaji wao mpya, Ntibazonkiza ataanza kuitumikia timu hiyo katika mechi yake ya kwanza kwenye Ligi Kuu tangu asajiliwe.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Klabu ya Dodoma Jiji, Mbwana Makata, alisema wataingia kwa tahadhari wakifahamu wanakutana na timu nzuri.

"Tumejiandaa vizuri kukutana na Yanga katika mchezo huo japokuwa wanaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu, tutapambana hivyo hivyo kupata matokeo," alisema Makata.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 9